BREAKING NEWS
SUPA JACKPOT
1,016,428,582/-
KWA 1000/- TU!
SportPesa.CO.TZ | PIGA *150*87#



UKURASA 3

**Jela** maisha kwa kumnajisi mtoto wa dada yake




UKURASA 11

Jumamosi Julai 23, 2022 • Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

# Nipashe

MWANGA WA JAMII

ISSN 0856 • Na. 0581015

www.ippmedia.com

www.twitter.com/nipashetz
www.facebook.com/nipashetz
www.instagram.com/theguardian_newspaper



Halima Mdee

# Hoja tatu za kesi mpya kina Mdee

**Walalamika** kortini kuitwa COVID-19... *Endelea ukurasa 2*



Rais Samia Suluhu Hassan na Rais wa Kenya, Uhuru Kenyatta, wakivuta pazia kuashiria ufunguzi wa Barabara ya Kikanda ya Afrika Mashariki yenye urefu wa kilomita 42.4, eneo la Ngaramtoni, jijini Arusha jana. Wanaoshuhudia ni Rais wa Uganda, Yoweri Museveni (wa nne kushoto), Rais wa Burundi, Évariste Ndayishimiye (wa tatu kushoto) na viongozi wengine. **PICHA: IKULU**

# Samia aagiza ulinzi wa miundombinu

UKURASA 2

UKURASA WA 3

## POLISI DAR WAWANASA WATUHUMIWA WA UJAMBAZI



JESHI la Polisi Kanda Maalum Dar es Salaam limewakamata watuhumiwa tisa kwa tuhuma za kujihusisha na...

UKURASA WA 4

## WASTAAFU WASIKILIZWA, WAIPONGEZA SERIKALI

BAADHI ya wastaafu kutoka Mkoa wa Dar es Salaam wamepongeza kasi ya utendaji wa serikali ya awamu ya sita kwa kuwasikiliza na kutatua...

UKURASA WA 4

## JAFO ATANGAZIA KIAMA WAMILIKI VIWANDA VILIVYOKAIDI AGIZO LA SERIKALI MAZINGIRA

WAZIRI wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira), Dk,. Selemani Jafo, amesema wamiliki wa viwanda...

## Bilioni 700/- kuhamisha wakazi wa Ngorongoro

UKURASA 3

MICHEZO SAKHO AWINDWA NA VIGOGO UK.24 | MAONI, KATUNI UK.6



Mhariri Mtendaji wa Gazeti la Nipashe, Beatrice Bandawe (kulia), akikata keki kusherehekea kutimiza miaka 60 ya kuzaliwa, iliyoandaliwa na kampuni ya The Guardian Ltd (TGL), inayochapisha magazeti ya The Guardian na Nipashe, Mikocheni, Dar es Salaam jana. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# Rais Samia aagiza ulinzi miundombinu

**Na Cynthia Mwilolezi,** ARUSHA

RAIS Samia Suluhu Hassan amewataka wananchi kuilinda na kuitunza miundombinu inayojengwa kwa gharama kubwa ili iendelee kudumu na kuimarisha uchumi wa nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki ( EAC).

Vilevile, amemhakikishia Rais Uhuru Kenyatta wa Kenya ambaye anamaliza muda wake wa uongozi kwamba mipango yote waliyojiwekea, ukiwamo ujenzi na miundombinu ya barabara, ataikamilisha kama walivyokubaliana kwenye vikao vyao.

Rais Samia aliyasema hayo jijini Arusha wakati wa hafla ya ufunguzi wa Barabara ya Kikanda ya Afrika Mashariki (Arusha Bypass) yenye urefu wa kilomita 42.4 iliyojengwa kwa thamani ya dola za Marekani milioni 217, Tanzania zikitumika dola milioni 212 na Kenya dola milioni 105.

Alisema ameona licha ya jitihada za ujenzi wa miundombinu unaofanywa na serikali pamoja na nchi za EAC, kumezuka tabia ya uharibifu wa miundombinu hiyo, ukiwamo wizi wa vyuma vya madaraja.

"Niwaombe sana Watanzania tuheshimu na kufuata taratibu zilizowekwa katika utunzaji wa barabara kwa sababu imezuka tabia ya baadhi ya watu kuharibu miundombinu ya barabara pamoja na kutengeneza magari barabarani na kumwaga mafuta machafu yanayosababisha kuharibu miundombinu ya barabara iliyotengenezwa kwa fedha nyingi," alisema.

Rais Samia alisema Serikali ya Tanzania inaendelea kutekeleza miradi mbalimbali ya miundombinu ya reli, barabara, usafiri wa anga na majini ili kuunganisha nchi za EAC.

Aliwataka wananchi ambao miundombinu hiyo inatekelezwa katika maeneo yao, kutumia fursa za ujenzi wa miundombinu hiyo kujikwamua kiuchumi.

Rais Samia pia alitumia fursa hiyo kuwataka Watanzania kujitokeza kwa wingi Agosti 23 mwaka huu kuhesabiwa katika Sensa ya Watu na Makazi ambayo itasaidia serikali kupanga mipango ya maendeleo kwa wananchi.

Pia aliwaasa wananchi kuendelea kuchukua tahadhari dhidi ya ugonjwa wa UVIKO-19 pamoja na kuchanja.

**RAIS KENYATTA**

Katika hafla hiyo, Rais Kenyatta aliwataka wananchi kuendelea kuunga mkono viongozi wa nchi za EAC ili waendelee kushirikiana kwa pamoja katika kuleta maendeleo kupitia umoja wao ambao utachochea heshima ya jumuiya hiyo kwa mataifa makubwa duniani.

"Ni ishara kubwa kuwa viongozi tukiungwa mkono tukashirikiana kwa pamoja, hakuna changamoto itakayotushinda, tutafanya maendeleo makubwa kupitia umoja wetu na kuheshimika na mataifa makubwa duniani," alisema.

Kuhusu barabara hiyo, Rais Kenyatta alisema itasaidia kuunganisha nchi wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki pamoja na kurahisisha usafiri wa bidhaa mbalimbali za mboga na mazao mengine ya biashara.

"Huu ni utajiri mkubwa wa fursa katika kukuza uchumi wa nchi wanachama hasa kwa wakulima wa Tanzania ambao gharama za kusafirisha mazao yao zitapungua kutokana na kuwapo wa barabara hii," alisema.

Kenyatta pia alitumia fursa hiyo kumpongeza Rais Samia ambaye alipokea nchi katika kipindi cha majonzi na watu wengi walikuwa na hofu, lakini amekuwa hodari na mchapakazi.

"Kuna msemo wa Kiswahili 'usimwone Simba amenyeshewa ukadhani ni paka'. Dada yangu Rais Samia alipokea nchi katika kipindi cha majonzi na wengi walikuwa na hofu, lakini amekuwa na ujasiri na mchapakazi," alipongeza.

Katibu Mkuu wa Jumuiya ya Afrika Mashariki, Dk. Peter Mathuki, alisema Afrika inahitaji kufikia mtengamano katika kukuza uchumi kwa kuwa na miundombinu imara na viwanda vya kutengeneza bidhaa zitakazokuza uchumi.

"Barabara hii ni muhimu katika kuimarisha biashara kwa nchi wanachama wa EAC. Hii ni hatua muhimu ya utengamano na inaongeza uhimilivu katika miundombinu ya barabara," alisema.

Alisema moja ya mipango ya EAC kujiimarisha kiuchumi ambapo wameweka vipaumbele vitano vilivyopewa msukumo mkubwa. Alivitaja vipaumbele hivyo kuwa ni usafiri wa anga, reli, Tehama, bandari na usafiri wa majini.

Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi wa Tanzania, Prof. Makame Mbarawa, alisema barabara hiyo itapunguza urefu wa safari kutoka Tanzania hadi Mombasa, Kenya.

Alisema barabara hiyo itafungua fursa nyingi za kiuchumi na kijamii kwa nchi wanachama, hasa Tanzania.

Mwakilishi Mkazi wa Benki ya Maendelek ya Afrika (AfDB) nchini, Patricia Laverley, alisema benki hiyo imetoa fedha hizo kwa ajili ya kusaidia maendeleo na kuimarisha uchumi kwa nchi za EAC.

Aliahidi kuendelea kushirikiana na nchi za EAC katika kutekeleza miradi ya maendeleo.

# Hoja tatu za kesi mpya kina Mdee

**Na Grace Gurisha**

HATIMAYE Mbunge wa Viti Maalum, Halima Mdee na wenzake 18 wamefungua shauri katika Mahakama Kuu Masjala Kuu kupinga kuvuliwa uanachama wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA) wakiomba amri tatu zitolewe.

Mdee na wenzake walifungua shauri hilo jana, likisajiliwa kwa namba 36/2022, wakiiomba mahakama hiyo ipitie mchakato na uamuzi wa kuwafukuza uanachama na kisha itoe amri tatu.

Katika shauri hilo, wabunge hao wanaiomba mahakama itengue mchakato na uamuzi wa kuwavua uanachama na pia iwalazimishe CHADEMA kuwapa haki ya kuwasikiliza.

Pia wanaomba kuwekwe zuio dhidi ya Spika wa Bunge la Tanzania na Tume ya Taifa ya Uchaguzi (NEC) kuchukua hatua yoyote hadi malalamiko yao yatakapotolewa uamuzi.

Pamoja na mambo mengine, wabunge hao wanadai kuwa mchakato na uamuzi wa kuwafukuza uanachama haukuzingatia matakwa ya kisheria na misingi ya haki - kwamba hawakupewa haki ya kusikilizwa.

Katika kiapo cha Mdee, anadai kuwa Novemba 25, 2020, CHADEMA walimtumia barua ya maelezo ya makosa yake kupitia mtandao wa WhatsApp na kumtaka ahudhurie kikao cha Kamati Kuu kilichopangwa kufanyika Novemba 27, 2020, ikiwa ni taarifa ya siku mbili tu.

"Kutokana na hasira na vitisho vya usalama na kauli za Katibu Mkuu wa CHADEMA kwa umma kuwa ni wasaliti, matokeo yake wanachama wa chama hicho walianza kutoa vitisho kwa kiwango cha kushutumiwa na hata kuitwa Covid- 19," Mdee anadai katika kiapo chake.

Mdee pia anadai kuwa kutokana na hayo, aliingiwa na hofu ya kushambuliwa na wanachama wa CHADEMA waliochochewa na kauli za viongozi wa chama hicho, akiwamo Katibu Mkuu, John Mnyika.

Anadai kuwa kutokana na hofu hiyo, kwa kuzingatia kuwa siku ya kupata wito wa kufika mbele ya Kamati Kuu, Dar es Salaam Novemba 27, 2020, akiwa jijini Dodoma, aliiandikia Kamati Kuu akiomba ahirisho la kikao hicho na kuongezwa muda.

Mdee anadai lengo lilikuwa ni kufanya hali ipoe na kujihakikishia usalama na pia kupata muda wa kutosha kujiandaa kwa usikilizwaji na kuwasilisha utetezi wake.

Anadai kuwa kutokana na nia ovu, ombi lake lilikataliwa na Kamati Kuu kupitia barua aliyotumiwa na Katibu Mkuu kupitia WhatsApp Novemba 26, 2020, hivyo shauri lake likasikilizwa na kuamuliwa upande mmoja.

"Nilikata rufani Baraza Kuu Desemba 23, 2020 nikipinga uamuzi huu wa Kamati Kuu na utaratibu wote uliotumika kwa kuwa sikupewa haki ya kusikilizwa na hivyo kukiukwa kwa haki yangu ya msingi," Mdee anadai katika hati hiyo.

Anadai sababu iliyotolewa na Baraza Kuu kumfukuza uanachama ilitokana na makosa yasiyo na maana na yasiyothibitika kuwa alikula njama kujiteua mwenyewe na wenzake na kuapa kuwa mbunge wa viti maalum.

Mdee anadai kwamba mara tu baada ya kula kiapo Novemba 24, 2020, Katibu Mkuu wa CHADEMA, Mnyika, alimtaja yeye na wenzake 18 kama wasaliti.

Anadai kuwa Mnyika alikwenda mbali alipowaalika wanachama wa CHADEMA na umma kwa kutoa mapendekezo kuhusu vikwazo vinavyofaa kuwawekea, hata kabla hajapewa barua au maelezo ya makosa yake na nafasi ya kusikilizwa na Kamati Kuu.

Uamuzi huo wa Baraza Kuu ulitokana na rufani walizozikata Mdee na wenzake kupinga uamuzi wa awali wa kuwavua uanachama uliotolewa na Kamati Kuu Novemba 27, 2020, iliyowatia hatiani kwa kosa la kwenda kuapishwa kuwa wabunge wa viti maalum bila ridhaa ya chama.

Katika shauri hilo, Mdee na wenzake wanawakilishwa na Mawakili Ipilinga Panya, Aliko Mwamanenge, Edson Kilatu na Emmanuel Ukashi.

# Polisi wawanasa watuhumiwa ujambazi

Na Romana Mallya

JESHI la Polisi Kanda Maalum Dar es Salaam limewakamata watuhumiwa tisa kwa tuhuma za kujihusisha na matukio ya ujambazi, wanadaiwa kwenda kufanya uhalifu katika ghala moja wilayani Temeke, Dar es Salaam.

Akizungumza na waandishi wa habari jana mkoani humo jana, Kamanda wa Kanda hiyo, Jumanne Muliro, alisema tukio hilo lilitokea usiku wa kuamkia jana kwenye kiwanda cha SHERI Automotive Germany kilichoko barabara ya Mbozi Keko wilayani Temeke.

Kamanda Muliro alisema Jeshi la Polisi lilipata taarifa ya kuwapo kwa wahalifu hao eneo hilo na walikuwa na bastola na mapanga.

Alisema baada ya watuhumiwa hao kuwabaini polisi, walianza kuwashambulia kwa risasi lakini askari walijihami na kuwakamata.

"Baada ya upekuzi, walikutwa na bastola moja iliyofutwa namba ikiwa imebakia na risasi tatu na silaha za jadi ambazo ni mapanga manne na funguo nyingi aina mbalimbali za kufungulia maghala na ofisi za kiwanda hicho," alisema.

Kamanda Muliro alisema wahalifu hao wakiwa ndani ya ghala hilo, walikutwa na gari aina ya Toyota Hiace lenye namba za usajili T201 DXN likiwa limepakiwa mali za wizi ambazo ni maboksi zaidi ya 70 ya vipuri," alisema.

Kiongozi huyo wa polisi alisema baadhi ya watuhumiwa hao wamepelekwa hospitali kwa matibabu ambapo baada ya kupata nafuu, watahojiwa.

"Jeshi la Polisi tunatoa onyo na tahadhari kuwa wahalifu waache kujihusisha na vitendo vilivyo kinyume cha sheria kwani tayari wamemsikia na kumwelewa Mkuu mpya wa Jeshi la Polisi nchini, kuwa anawataka askari watumie mbinu zote kuzuia na kukabiliana na vitendo vya kihalifu huku wakizingatia haki na sheria," alisema.

# Bil. 700/- kuhamisha wakazi wa Ngorongoro

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

MAMLAKA ya Hifadhi ya Ngorongoro (NCAA) imesema Sh. bilioni 700 zinatarajiwa kutumika kuwahamisha wananchi walioko kwenye hifadhi hiyo.

Vilevile, serikali inaendelea kutafakari namna bora ya kuhifadhi eneo hilo, ikisisitiza kuwa suala la kuwaondoa kwa nguvu halipo.

Akizungumza jana na waandishi wa habari jijini hapa kuhusu utekelezaji wa shughuli za NCAA na mwelekeo wa mwaka 2022/23, Naibu Kamishna wa Uhifadhi wa Mamlaka hiyo, Dk. Christopher Timbuka, alisema gharama hiyo ni kulingana na idadi ya kaya 22,000 zilizoko kwa sasa Ngorongoro.

"Lengo letu kubwa ni ikolojia ya hili eneo itunzwe, na utaratibu wa baadaye tutaendelea kuelimisha wananchi, ambao wapo tayari wataendelea kuhama na kuhama siyo lazima kwenda eneo la Msomera, serikali imesema hata kama mtu anataka kuhamia eneo lingine ni rukhsa, atalipwa stahiki zake na kwenda kwenye eneo analotaka," alisema.

Kiongozi huyo alisema kumekuwapo na mwitikio mkubwa wa watu kuhama kwa hiari ambapo ndani ya miezi miwili hadi Julai 18, mwaka huu tayari kaya 757 zenye watu 4,344 zimejiandikisha huku wakipewa fedha za kianzio ili kujikimu katika maisha yao na wataendelea kupata huduma kwa miezi 18.

"Ukiondoa fedha wanazolipwa kama fidia kwa maendeleo waliyoyafanya kule ndani na mali zisizohamishika, pia wanapewa fedha nyingine ili kuanza kujitegemea, na serikali ilisema mazao yanatumia miezi sita kuvunwa, sasa kutokana na kuandaa shamba hadi kuvuna serikali itawahudumia wale wananchi kwa miezi 18, tunaamini baada ya miezi hiyo watakuwa wamevuna mazao yao," alisema.

Naibu Kamishna huyo alisema idadi ya mifugo ambayo imeandikishwa kuondolewa ni 8,276 na serikali inazingatia uhamaji wenye staha.

"Mwaka 2018 hdi 2020 serikali iliunda tume kupitia changamoto za hifadhi na kuangalia namna ya kupunguza athari, na kati ya masuala yaliyojitokeza kwa wananchi walihitaji kumilikishwa ardhi.

"Walitaka kufanya kilimo na shughuli za kibiashara kama maeneo mengine. Sasa kwa Sheria ya Ngorongoro, hii ni ngumu, ndiyo ukaja uamuzi wa kuwahamisha kwa hiari ili kulinda hifadhi, na serikali ikawapeleka Msomera ili wapate maendeleo wanayohitaji," alisema.

Alipoulizwa kuhusu muda wa kuhama, kiongozi huyo alisema mamlaka inatamani kuwe kwa muda mfupi lakini kuna gharama na wanakadiria kuhama kutafanyika kwa miaka mitatu.

"Kinachofanyika kule ni ujenzi wa nyumba na zinajengwa kwa awamu. Kwa hiyo, tunategemea kwamba wananchi watakaopenda kwenda kule hadi sasa tumefikia 700 lakini tunategemea ndani ya muda mfupi kupeleka 500, na linafanyika zoezi hili kulingana na bajeti," alisema.

Aliongeza kuwa serikali haijasema kuhusu wasiotaka kuhama isipokuwa wahifadhi wanashauri idadi ya watu ipunguzwe kwenye eneo hilo.

"Sababu ya kutaka idadi ya watu ipunguzwe, kuna taarifa ambazo sikuzisema NBS (Ofisi ya Taifa ya Takwimu) walifanya sensa katika lile eneo.

"Kati ya vitu walivyobaini ni kwamba lile eneo lina umaskini wa hali ya juu, pia lina kiasi kukubwa cha wasiojua kusoma na kuandika, kipo kwenye asilimia 64 na kilichosababisha watoto wasiende shule ni kutokana na mazingira ya hifadhini, siyo rahisi mtoto atoke saa 12 asubuhi awahi shuleni kutokana na wanyama wakali wengi," alisema.

Akieleza baadhi ya mafanikio waliyoyapata katika mamlaka hiyo, Dk. Timbuka, alisema kwa wiki tatu za mwanzo wamefanikiwa kuongeza watalii na mapato ambapo watalii 39,900 kutoka nje na watalii 18,000 wa ndani na Sh. bilioni 20.1 zimekusanywa.

**MWELEKEO WA MAMLAKA**

Dk. Timbuka alisema mamlaka imejipanga kutangaza zaidi vivutio ikiwamo mchanga unaohama ambao ni mfumo wa Ikolojia wa Ngorongoro na kwamba ni eneo la pili Afrika baada ya Morocco.

Alisema mwelekeo wa mwaka 2022/23 ni kuongeza idadi ya watalii kufikia milioni 1.2 na sehemu za malazi 480 ili kuwa na maeneo ya wageni kulala ambapo wametoa maeneo mapya sita ya uwekezaji wa hoteli kwenye eneo hilo.

Msemaji Mkuu wa Serikali, Gerson Msigwa, aliwataka waandishi wa habari kuandika habari za Ngorongoro kutoka kwenye vyanzo sahihi vya habari.

"Serikali bado inatafakari namna bora ya uendeshaji wa Hifadhi ya Ngorongoro," alisema.



Wafanyabiashara wadogo maarufu Machinga, wamerudi tena na kufanya biashara zao, kwenye njia ya waenda kwa miguu, eneo la Kimara Mwisho, Manispaa ya Ubungo, mkoani Dar es Salaam jana, licha ya serikali kupiga marufuku ufanyaji wa biashara katika maeneo yasiyoruhusiwa. **PICHA: SABATO KASIKA**

# Afungwa jela maisha kwa kulawiti kubaka mpwa wake

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

MAHAKAMA ya Wilaya ya Chunya mkoani Mbeya imemhukumu kifungo cha maisha jela, Change Mawanga (32), mkazi wa Kijiji cha Mlima Njiwa Kata ya Mbugani wilayani humo kwa kosa la kumbaka na kumlawiti mtoto wa dada yake mwenye umri wa miaka minne.

Aidha, kijana huyo anadaiwa kumwambukiza mtoto huyo magonjwa ya zinaa.

Hukumu hiyo ilitolewa juzi na Hakimu Mkazi Mfawidhi wa Mahakama ya Wilaya ya Chunya, James Mhanusi, baada ya kusikiliza pande zote mbili na kujiridhisha pasi na shaka kuwa mshtakiwa alitenda kosa hilo.

Awali, akisoma mashtaka katika kesi hiyo ya jinai namba 64 ya mwaka 2022, Mwendesha Mashitaka wa Polisi, Mazoya Luchagula, aliiambia mahakama kuwa mshtakiwa alitenda makosa hayo kwa nyakati tofauti kati ya Aprili na Mei 5, mwaka huu.

Mazoya alisema makosa hayo ni kinyume cha kifungu namba 130(1)(2) na kifungu namba 131(1), Sura ya 16 ya Sheria ya Makosa ya Jinai iliyofanyiwa marejeo mwaka 2019.

Mtuhumiwa alikana mashtaka yote na ndipo upande wa mashtaka ukalazimika kuleta mashahidi mbalimbali mahakamani hapo.

Miongoni mwa mashahidi waliofikishwa mahakamani hapo pamoja na mtoto aliyefanyiwa ukatili huo, ambaye alimtambua mshtakiwa kwa kumwita 'anko' (mjomba).

Mashahidi wengine wa mashtaka waliotoa ushahidi wao mahakamani hapo ni mama mzazi wa mtoto, askari, ofisa ustawi wa jamii wa wilaya na daktari aliyewasilisha fomu ya polisi namba tatu (PF3) iliyoambatana na vipimo vilivyoonesha mtoto kubakwa na kuingiliwa kinyume cha maumbile.

Baada ya Hakimu Mhanusi kusikiliza upande wa mashtaka na upande wa mshtakiwa, alisema mahakama iliridhika na ushahidi uliotolewa na upande wa mashtaka na kwamba mshtakiwa ana kesi ya kujibu.

Akijitetea mbele ya mahakama hiyo, mshtakiwa Mawanga alidai kuwa hakutenda makosa hayo na kwamba anasingiziwa, huku akiiomba mahakama kumwachia huru kwa kuwa mama yake, mke na wadogo zake wanamtegemea.

Upande wa mashtaka ulidai kuwa licha ya mshtakiwa kutokuwa na matukio mengine ya uhalifu, unaiomba mahakama kutoa adhabu kali kwa mshtakiwa ikizingatiwa mtoto aliyefanyiwa ukatili ana umri wa miaka minne na isitoshe ni mtoto wa dada yake.

Hakimu Mhanusi baada ya kuzisikiliza pande zote, alisema Mahakama inamtia hatiani kwa makosa yote mawili, ya kumbaka mtoto chini ya miaka 18 na kumlawiti ambayo kifungo chake ni cha maisha jela.

Hakimu Mhanusi alisema adhabu hiyo iwe fundisho kwa mshtakiwa na watu wengine wanaojihusisha na vitendo hivyo hasa kutokana na kukithiri ubakaji na ulawiti kwa watoto wilayani Chunya.

Vitendo vya ulawiti na ubakaji wa watoto wilayani Chunya vinahusishwa na imani za kishirikina kwa madai kuwa watu wanaweza kupata dhahabu punde wanapojamiiana au kuwalawiti watoto wadogo.

Hakimu Mhanusi alisema kwa makosa yote mawili mshtakiwa atatumikia adhabu zote mbili kwa pamoja gerezani.

# NMB yamwaga misaada mabati, madawati Mbeya

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

BENKI ya NMB imekabidhi msaada wa mabati 600 na madawati 500 wenye thamani ya Sh. milioni 70 kwa ajili ya shule tano za Jiji la Mbeya.

Msaada huo ulikabidhiwa juzi na Ofisa Mkuu wa Wateja Binafsi na Biashara wa NMB, Filbert Mponzi, katika hafla maalumu iliyofanyika katika Shule ya Sekondari Iduda na kupokewa na Spika wa Bunge, Dk. Tulia Akson.

Mponzi alisema msaada huo unalenga kuzinufaisha shule tatu za sekondari na mbili za msingi na kwamba benki hiyo iliamua kutoa msaada huo kutokana na maombi maalumu yaliyotolewa na viongozi wa shule hizo.

Alizitaja shule zitakazonufaika na msaada huo kuwa ni za sekondari Iduda, Itende na Itagtano ambazo kila moja itapewa mabati 200 na madawati 100 pamoja na shule za msingi Inyala na Ikuti ambazo zitapatiwa madawati 100 kila moja.

Mponzi alisema mbali na msaada huo, benki hiyo imekuwa na utaratibu wa kutoa misaada mingine kama hiyo kwa ajili ya kushirikiana na serikali kutatua upungufu wa madawati na miundombinu mingine ya shule pamoja na huduma za kijamii.

"NMB tumekuwa na utaratibu wa kuchangia huduma za kijamii na tumejikita zaidi kwenye maeneo ya afya, elimu na misaada ya hali na mali katika nyakati ngumu kama za majanga.

"Misaada ambayo tunatoa lengo huwa ni kurejesha sehemu ya faida yetu kwa jamii ambapo utaratibu huu tumeufanya kwa muda wa miaka tisa mfululizo na tumekuwa tukitenga asilimia moja kila mwaka," alisema.

Mwaka huu, alisema benki hiyo imetenga Sh. bilioni mbili kwa ajili ya kutoa misaada kwenye sekta hizo za elimu, afya na maeneo ya majanga kwahiyo tunakaribisha maombi mengine kwenye maeneo haya.

Mponzi alisema Mbeya ni miongoni mwa mikoa nchini ambayo imekuwa ikinufaika zaidi na misaada ya benki hiyo. Alisema katika kipindi cha miaka miwili, mkoa huo umepata msaada wa zaidi ya Sh. milioni 300.

Alisema kati ya fedha hizo, Sh. milioni 100 zimenufaisha sekta ya elimu na Sh. milioni 200 kwenye sekta ya afya.



Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu, Profesa Joyce Ndalichako akizungumza na wastaafu wa Mkoa wa Dar es Salaam aliokutana nao jana kwa ajili ya kusikiliza na kutatua kero zao. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Wastaafu wasikilizwa, waipongeza serikali

**Na Mwandishi Wetu**

BAADHI ya wastaafu kutoka Mkoa wa Dar es Salaam wamepongeza kasi ya utendaji wa serikali ya awamu ya sita kwa kuwasikiliza na kutatua changamoto mbalimbali zinazowakabili.

Walikuwa wakizungumza kwa nyakati tofauti wakati wa mkutano na Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu, Profesa Joyce Ndalichako, wenye lengo la kusikiliza na kutatua changamoto zinazowakabili wastaafu wanaohudumiwa na Mifuko ya Hifadhi ya Jamii wa NSSF na PSSSF.

Wastaafu hao waliishukuru serikali chini ya uongozi wa Rais Samia Suluhu Hassan kwa kuonyesha dhamira ya dhati ya kushughulikia changamoto mbalimbali zinazowakabili jambo ambalo limewajengea imani kwa serikali yao.

"Kwa kweli tunamshukuru kwa dhati Rais Samia kwa kumtuma Waziri Ndalichako kuja kusikiliza kero za wastaafu hii haijawahi kutokea," alisema Anna Malisa.

Alisema katika mkutano huo kila mstaafu aliwasilisha kero yake mbele ya Waziri Ndalichako ambaye kwa kushirikiana na watendaji wa Mifuko ya NSSF na PSSSF walizitatua na kuzipatia ufumbuzi.

Naye, Chuki Kashaija, alisema wana imani kubwa na serikali yao kwa kuonyesha dhamira njema ya kusikiliza na kutatua kero mbalimbali zinazowakabili wastaafu nchini.

Kwa upande wake mstaafu Aulerian Ndumbai, alipongeza kazi kubwa na nzuri inayofanywa na Rais Samia ya kuwahudumia wananchi hususan katika kufuatilia na kutatua kero zao baada ya kulitumikia taifa kwa muda mrefu.

"Sisi wastaafu tunasema hatuna cha kumlipa Mama Samia ametufanyia jambo kubwa hili halijawahi kufanyika kwa miaka mingi yeye amemtuma Waziri Ndalichako aje atusikilize kwa niaba yake tunampongeza sana kwa kazi kubwa anayofanya," alisema.

Alisema kupitia mkutano huo wa Waziri Ndalichako walisikilizwa na kutatuliwa kero zao mbalimbali na waliwaomba wananchi kuendelea kuunga mkono kazi kubwa inayofanywa na serikali.

Akizungumza na wastaafu hao, Waziri Profesa Ndalichako alisema lengo la mkutano huo ni maelekezo ya Rais Samia ya kutaka wasaidizi wake kuhakikisha wanatatua kero ambazo ziko katika maeneo yao.

Wasaidizi wake lazima wahakikishe wanatatua kero ambazo ziko katika maeneo yao.

"Na mimi Mheshimiwa Rais amenipatia kundi ambalo analiheshimu sana ni mama ambaye ana heshima kwa wazee na hataki kusikia wazee wakihangaika, Mheshimiwa Rais hataki kusikia wazee ambao wamelitumikia taifa hili kwa weledi, wametufikisha hapa tulipofika halafu leo hii wanasumbuliwa kwa vitu ambavyo ni stahiki yao," alisema Waziri Profesa Ndalichako.

Katika mkutano huo Waziri Ndalichako alikutana na kusikiliza pamoja na kutatua kero za wastaafu zaidi ya 1,000.

# Jafo atangazia kiama wamiliki viwanda vilivyokaidi agizo la serikali mazingira

**Na Joseph Mwendapole**

WAZIRI wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira), Dk. Selemani Jafo, amesema wamiliki wa viwanda ambao wameshindwa kutekeleza maagizo ya serikali kuhusu uchafuzi wa mazingira siku zao zinahesabika na yeye si waziri wa kupenda kukaa ofisini.

Ameliagiza Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira (NEMC), kushughulika na viwanda hivyo.

Jafo alisema hayo jana baada ya kutembelea kiwanda cha chuma cha Iron & Steel cha Mikocheni, Dar es Salaam huku akisema serikali haiwezi kuvumilia kiwanda kinachochafua mazingira na kushindwa kutekeleza maagizo, hivyo kuitaka NEMC kuwashughulikia. Waziri Jafo alitembelea kiwanda hicho kujionea utekelezaji wa maagizo aliyoyatoa mwaka jana ya kuzuia moshi unaotoka kwenye kiwanda ambao ulikuwa unalalamikiwa na wakazi wa eneo hilo.

"Mimi si waziri wa kukaa ofisini. Ni waziri wa 'field', nimetembelea viwanda vingi na asilimia 90 ya tuliowapa maagizo wametekeleza na NEMC si ile ya zamani mliyokuwa mnasema haina meno. Hii ya sasa itawashughulikia," alisema Jafo. Pia alisema amefurahishwa kwa wamiliki wa kiwanda hicho walivyotekeleza maagizo yote ya serikali na kuwataka wengine wote kuiga mfano huo.

"Kiwanda hiki ni mfano wa kuigwa nchi nzima. NEMC nendeni nchi nzima mkaangalie wale ambao wakipewa maagizo ya serikali wanasuasua kuyatekeleza na kama muda tuliowapa umekwisha wachukulieni hatua," alisema Jafo.

Alisema amefurahi kuona wamejenga kivuli sehemu ya kutunzia vyuma chakavu, ukuta wa kuzuia maji taka yasiathiri makazi ya watu na namna walivyomudu kuzuia moshi uliokuwa unatoka na unaathiri watu.

"Nakupongeza Mkuu wa Wilaya ya Kinondoni na timu yako. Nakumbuka nilikuja hapa baada ya kupata malalamiko ya watu wa Mikocheni kuhusu moshi na niliitoa maagizo nikiwa na wewe nilisema sitawapa kibali cha kukusanya taka hatarishi mpaka watekeleze maagizo.

"Nashukuru DC umekuwa ukifuatilia maagizo haya na sasa natamka hapa baada ya watu wangu wa NEMC kuja na kunihakikishia kwamba wametekeleza nilishasaini kibali chao waendelee na kazi na kama kuna changamoto waje," alisema.

Jafo alisema wawekezaji wa kiwanda hicho ni watu wa kuigwa kwa namna ambavyo wamekuwa wakitekeleza maagizo ya serikali kwani wengine wamekuwa wakiyatekeleza kwa kusuasua.

Mkuu wa Wilaya ya Kinondoni, Godwin Gondwe, alisema wananchi wa eneo hilo walikuwa wakilalamikia moshi na utiririshaji wa maji taka lakini baada ya maagizo ya Waziri wamefanikiwa kurekebisha.

"Baada ya Waziri kuja hapa na kutoa maagizo nilikuwa nakuja hapa kufuatilia na kwa kweli binafsi nimefurahi sana baada ya kuona wametekeleza maagizo yote manne. Sasa wengine wajiandae kwa sababu sisi hatutalala," alisema.

## Wapewa mwezi mmoja kupima maeneo ya serikali

**Na Thobias Mwanakatwe,** SINGIDA

MAOFISA Ardhi katika halmashauri za mkoa wa Singida wamepewa mwezi mmoja kuhakikisha wanapima taasisi zote za serikali ili kukabiliana na tatizo la uvamizi unaofanywa na baadhi ya watu.

Katibu Tawala Mkoa wa Singida, Dorothy Mwaluko, alitoa agizo hilo jana kwenye kikao kazi cha watumishi wa sekta ya ardhi mkoa kilichofanyika mjini hapa.

"Maofisa ardhi mliopo kwenye halmashauri kapimeni taasisi zote za serikali ili maeneo yote yawe na hati, hivi sasa taasisi nyingi zikiwamo shule zinavamiwa kwasababu hazijapimwa na nyie mpo mnaangalia tu," alisema.

Mwaluko alisema migogoro yote ya ardhi kati ya kijiji na kijiji, wilaya kwa wilaya na mkoa kwa mkoa iorodheshwe ifahamike ili hatua za kuipatia ufumbuzi ziweze kuanza haraka.

Aliongeza kuwa migogoro ya ardhi kwenye halmashauri tafsiri itolewe ili kufanyiwa kazi na ile ya mipaka ushauri wa kitaalam utolewe kwani hakuba sababu ya kukaa na migogoro bila kuitafutia ufumbuzi.

Naye Kamishina Msaidizi wa Ardhi Mkoa wa Singida, Shamimu Hoza, alisema baadhi ya maofisa ardhi wamekuwa kikwazo kutokana na tabia ya kuivaa migogoro badala ya kutoa ushauri.

"Wataalam hatutaki kutoa ushauri wa kuitatua migogoro, tuache tabia ya kuivaa migogoro, tuhakikishe GN zinapatikana," alisema.

Alisema suala la migogoro linafahamika kwa watalaam wote wa ardhi hivyo jukumu lao kubwa ni kutafsiri GN na sio kwenda kueleza wananchi kutafsiri mipaka.

# Wanaodaiwa kukusanya mil. 350/- za mapato halmashauri matatani

**Na Thobias Mwanakatwe,** IRAMBA

WATUMISHI 20 kati ya 52 wa Halmashauri ya Wilaya ya Iramba mkoani Singida waliotuhumiwa kukusanya zaidi ya Sh. milioni 353 za mapato ya ndani na kushindwa kuziingiza kwenye mfumo wa kibenki, wameanza kuchukuliwa hatua za kisheria.

Aidha, watumishi wengine wanne wa Hospitali ya Wilaya Kiomboi nao wameingia matatani baada ya kubainika wamekuwa wakiwatoza fedha na kuwadai rushwa wajawazito wanaokwenda kujifungua katika hospitali hiyo.

Kuanza kuchukuliwa hatua watumishi hao kunatokana na agizo lililotolewa na Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa, alipofanya ziara wilayani hapa Julai 16, mwaka huu, na kubaini ufisadi unaofanywa na baadhi ya watumishi wasio waaminifu katika halmashauri hiyo.

Mkuu wa Wilaya ya Iramba, Suleiman Mwenda, akizungumza na watumishi wa halmashauri hiyo jana, alisema baada ya maagizo ya Waziri Mkuu, iliundwa kamati ya kuchunguza mambo kadhaa yaliyolalamikiwa ikiwamo suala la fedha zilizokusanywa lakini hazikupelekwa benki.

Alisema katika uchunguzi huo imebainika watumishi 17 ambao ni kati ya 52 waliotuhumiwa mashtaka yao yamethibitika kwamba walikusanya mamilioni ya shilingi lakini hawakuziingiza kwenye mfumo wa mapato ya halmashauri.

"Tunaziachia mamlaka zingine ziendelee na utaratibu wa kuwachukulia hatua na pia tunamwagiza Mkurugenzi (Mtendaji) wa Halmashauri ya Wilaya achukue hatua za kinidhamu," alisema.

Mwenda alisema watumishi wengine watatu ambao wamefunguliwa mashtaka ambayo yatarudiwa na taratibu za kurejea mashtaka hayo zifuatwe.

Aliongeza kuwa watumishi 13 kamati imebaini kuwa mashtaka yao hayajathibitika kutokana na fedha walizokuwa wakidaiwa walishazirudisha lakini madeni yao bado hayajaondolewa kwenye mfumo wa mapato wa halmashauri.

"Tunamwagiza mkurugenzi afuatilie ajiridhishe kama kweli watumishi hao wamelipa madeni hayo ili waondolewe kwenye orodha ya wadaiwa.

Mwenda alisema watumishi wengine watatu, walikataa kupokea barua ya kuitwa kwenye kamati ya uchunguzi.

" Naagiza OCD (Mkuu wa Polisi wa Wilaya) watafutwe na kukamatwa mahali popote walipo na barua zao watakabidhiwa wakiwa chini ya ulinzi wa polisi," alisema.

Kuhusu watumishi wa sekta ya afya, alisema kamati ya uchunguzi imebaini walikuwa wakiwatoza fedha wajawazito,kuwaomba rushwa,nguo na huduma ya uchunguzi ya Ultrasound na gharama nyingine kinyume cha utaratibu.

Mkuu huyo wa wilaya aliwataja watumishi hao kuwa ni Mhoja Mpenda, Lisa Ngwesheni, Magreth Dilu na Peter Boniventure.

"Watumishi hao wamekuwa wakiwaomba rushwa na kuwalipisha wajawazito fedha kwa ajili ya huduma za kujifungua kikiwemo kipimo cha ultrasound," alisema.

Mwenda alisema watumishi hao hatua itakayochukuliwa dhidi yao ni kupewa onyo kali la kimaandishi kwa mujibu wa sheria ili wapate nafasi ya kujieleza na kujitetea juu ya tuhuma zinazowakabili.

Waziri Mkuu Majaliwa alipofanya ziara wilayani Iramba Julai 16, mwaka huu, wananchi wa mji wa Misigiri waliandika mabango ya malalamiko yakiwamo yaliyohusu wajawazito kutozwa fedha katika Hospitali ya Wilaya Kiomboi.



Mkuu wa wilaya ya Kishapu, Joseph Mkunde, akitoa elimu kwa jamii ya wafugaji wa kijiji cha Magalata, wilayani humo juzi, ili kuruhusu shughuli za utafiti wa mafuta ziendelee kwenye maeneo yao kutoka Shirika la Maendeleo la Mafuta ya Petroli Tanzania (TPDC). **PICHA: MARCO MADUHU**

# Vyuo vikuu vyahimizwa kuanzisha madawati jinsia ifikapo Desemba

**Na Mwandishi Wetu,** DODOMA

VYUO vikuu na vya kati nchini ambavyo havina madawati ya jinsia vimetakiwa kuhakikisha kufikia Desemba viwe vimeanzisha vitengo hivyo.

Naibu Katibu Mkuu Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum, Amon Mpanju, alitoa agizo hilo jana wakati akizindua dawati la jinsia katika Chuo Kikuu cha Dodoma (UDOM).

Mpanju ambaye aliambatana na Naibu Katibu Mkuu Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia, Prof. James Mdoe, aliomba wizara hizo kushirikiana kuhakikisha madawati 612 yanaanzishwa katika vyuo hadi ifikapo Desemba.

"Tusisubiri wabia watufadhili ndiyo tuzindue. Kufikia Desemba vyuo vikuu na vyuo vya kati vyote viwe na madawati kwa rasilimali zilizopo kwa sababu mwongozo upo na lengo ni kutoa wahitimu waliofuzu bila kuathiriwa na vitendo vya ukatili au unyanyasaji wa kijinsia," alisema.

Mpanju alipongeza UDOM kwa kuwa na utaratibu wa kupinga vitendo vya unyanyasaji wa kijinsia kabla hata ya mwongozo wa wizara wa uanzishwaji wa madawati hususani kaulimbiu inayowataka kutovumilia unyanyasaji huo na kuvitaka vyuo vingine kuiga mfano huo.

"Kuwa na sera na miongozo ya kupinga vitendo vya ukatili kabla ya uzinduzi wa dawati kunadhihirisha utayari wa chuo hiki kupambana na vitendo vya ukatili wa kijinsia," alisema Mpanju.

Alilishukuru pia Shirika la Umoja wa Mataifa la Elimu, Sayansi na Utamaduni (UNESCO) kwa kusaidia uzinduzi wa madawati 15 pamoja na kuona ukubwa wa chuo na kuamua kuzindua madawati mawili.

Naye Prof. Mdoe alisema wizara yake ilishatoa maelekezo ya kuwa na sera na miongozo vyuoni pamoja na kuanzisha madawati ya jinsia, hivyo watahakikisha wanasimamia vyuo hivyo ili vianzishe madawati hayo na yatumike kama mwongozo unavyokusudia.

"Sote tunakubaliana kuwa yakiwapo manyanyaso ya kijinsia, wanafunzi hawawezi kutimiza malengo yao, hivyo nielekeze vyuo vingine kuanzisha madawati haya kwa namna yoyote iwe kwa kushirikiana na wadau au kwa kutumia rasilimali za ndani," alisisitiza Prof. Mdoe.

Mwakilishi wa UNESCO, Mathias Herman, alisema shirika hilo linatambua juhudi zinazofanywa na Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia hasa katika kutoa miongozo ya uanzishwaji wa madawati ya jinsia na kuisimamia kuhakikisha inafanya kazi.

Mathias alisema madawati haya si tu kwamba yanazinduliwa bali yanakuwa na tija kwa kuwasaidia jumuiya yote ya wanachuo kutoa taarifa ya vitendo vya ukatili wa kijinsia na hatimaye kutokomeza vitendo hivyo katika taasisi hizo.

Akizungumza katika hafla hiyo, Makamu Mkuu wa UDOM, Dodoma Prof. Faustine Bee, alisema uanzishwaji wa dawati hilo chuoni hapo utasaidia kuongeza ufanisi wa kitengo cha jinsia kilichoanzishwa mwaka 2009 chuoni hapo.

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Adhabu dhidi ya Manara iwe fundisho kwa wadau

**SHIRIKISHO** la soka Tanzania (TFF), juzi lilitangaza kumfungia Msemaji wa Yanga, Haji Manara, kutojihusisha na masuala ya mpira kwa muda wa miaka miwili. Sambamba na adhabu hiyo, msemaji huyo ametozwa pia faini ya Sh. milioni 20.

Adhabu hiyo iliyotolewa na Kamati ya Maadili ya TFF, inatokana na Manara kubainika kufanya vitendo visivyo vya kiungwana na ukiukwaji wa maadili jambo ambalo halitakiwi katika mchezo wa soka.

Manara alitiwa hatiani kwa kumdhalilisha Rais wa Shirikisho hilo, Wallace Karia, baada ya kumtamkia maneno makali yenye mwelekeo wa utovu wa nidhamu wakati wa mechi ya fainali ya Kombe la Shirikisho la Soka la Azam kati ya Yanga na Coastal Union, iliyofanyika Julai 2, mwaka huu, katika Uwanja wa Sheikh Amri Abeid, Arusha.

Kutokana na kauli hiyo, sekretarieti ya TFF iliwasilisha malalamiko mbele ya kamati ya maadili ambayo kwa mujibu wa maelezo yaliyotolewa wakati wa hukumu, Manara alikiri kutamka, kuomba radhi.

Katibu wa Kamati hiyo, Walter Lungu, akisoma uamuzi, alisema Manara alipewa adhabu hiyo na faini, kulingana na Kanuni ya katiba ya TFF, kifungu cha 73(5) na (6) licha ya kwamba aliomba msamaha kutokana na kitendo alichofanya.

Hii si mara ya kwanza kwa Manara kukumbwa na adhabu ndani ya TFF kwani amekuwa akifanya mambo kama hayo mara kwa mara na kupewa adhabu kwa mujibu wa kanuni zinazoongoza soka nchini.

Kwa adhabu hiyo, Yanga itakosa huduma za msemaji wao huyo kuanzia sasa hasa katika matukio makubwa yanayokuja, likiwamo la Wiki ya Wananchi, ambayo huandamana na masuala mbalimbali ya kijamii pamoja na kutambulisha kikosi kipya kwa msimu mpya wa ligi.

Sambamba na klabu kukosa huduma zake, umma wa wapenda soka watakosa uwapo wake hasa kutokana na hamasa ambazo amekuwa akifanya na kuwavuta mashabiki wa soka kupenda mpira. Bila kuwapo kwa unazi wa namna yoyote, ni ukweli ulio wazi kwamba Manara amekuwa kivutio kikubwa katika kuhamasisha mambo ya soka hususani linapokaribia pambano la watani wa jadi, Simba na Yanga.

Awali, Manara alipokuwa Simba, alikuwa anawafanya mashabiki na wapenzi wa timu hiyo kutega masikio atatoa kauli gani na hata alipohamia upande wa pili, alikuwa kivutio kwa kuipamba timu yake na watu kumiminika uwanjani kushuhudia mchezo.

Baada ya kutangazwa kwa adhabu hizo, kumekuwa na maoni kinzani kutoka kwa wadau huku baadhi wakisema adhabu hiyo ni kubwa na imetolewa kwa uonevu huku wengine wakisema kutokana na kujirudia mara kwa mara kwa matendo kama hayo anayoyafanya, anastahili na huenda ni ndogo kuliko iliyotarajiwa.


Pamoja na hayo yote, vitendo kama hivyo, tena vya udhalilishaji dhidi ya viongozi wa juu waliopewa dhamana ya kusimamia maendeleo ya soka nchini, adhabu aliyopewa ni sahihi kwa minajili ya kulinda heshima kwa mamlaka zilizokasimiwa jukumu la kuendeleza mchezo huo ambao unapendwa na mabilioni ya watu duniani.

Inawezekana kulikuwa na sababu ya yeye kufanya hivyo lakini kulingana na mazingira na kitendo kilichofanyika, ni dhahiri kwamba adhabu hiyo ni sahihi na kwa sasa inapaswa kuheshimiwa. Kutokana na ukweli kwamba soka ni 'fair play', Manara alistahili kuwa mvumilivu hata kama alichokozwa kwa namna yoyote.

Wanaopinga kwamba Manara ameonewa, wakiwamo wanachama wa Yanga na wadau mbalimbali kama vile wachambuzi wa michezo katika vyombo vya habari, wanapaswa kukubaliana na uamuzi huo ambao umetolewa kwa mujibu wa sheria na kanuni zilizowekwa, hivyo ni vyema wakasubiri kama matokeo mengine iwapo mhusika atakata rufani.

Kuna msemo kwamba "atajifunzaje asipochafuka?" Kwa mantiki hiyo kuna uwezekano mkubwa adhabu hiyo ikaleta sura mpya katika utendaji kwenye medani ya soka kwani ni imani kwamba kupitia adhabu hiyo watu watajifunza kuheshimu mamlaka zilizowekwa kwa mujibu wa sheria na kanuni za taasisi pamoja na nchi kwa ujumla.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
**THE GUARDIAN LIMITED**
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge



Na Adam Fungamwango

# Tujifunze kuheshimu mamlaka za michezo

**KAMATI** ya Maadili ya Shirikisho la Soka Tanzania (TFF) juzi ilitangaza kumhukumu Msemaji wa Yanga, Haji Manara kifungo cha miaka miwili kutojihusisha na soka ndani na nje ya nchi, pamoja na kulipa faini ya Sh. milioni 20.

Manara alikutwa na hatia katika shauri lililowasilishwa kwenye kamati hiyo na sekretarieti ya TFF kwa kosa la kumtolea kauli za vitisho Rais wa shirikisho hilo, Wallace Karia kwenye mechi ya fainali ya Kombe la FA, kati Yanga dhidi ya Coastal Union Julai 2, mwaka huu kwenye Uwanja wa Sheikh Amri Abeid jijini Arusha.

Katibu wa kamati hiyo, Walter Lungu alisema hukumu hiyo imetolewa kwa mujibu wa kanuni zilizowekwa.

Kumekuwa na mjadala mkali juu ya Manara kufungiwa, wengine wakidai ameonewa na wengine wakisema amestahili.

Wapo wanaoona ni kweli amekosea lakini adhabu aliyopewa ni kubwa, lakini kuna wanaoona adhabu hiyo ni ndogo kulingana na kosa alilofanya.

Kuna wanaotaka asamehewe, lakini wapo wanaotaka iendelee ili kuwafanya wengine wenye mawazo kama hayo kuogopa kufanya hivyo.

Nimesikia baadhi ya wachambuzi na wadadisi wakidai Manara amefanya hivyo kwa sababu huenda amechokozwa.

Na wanataka kwanza waangalie chanzo ni nini hadi kufanya hivyo. Ina maana hawa wakipata chanzo kama atakuwa amechokozwa basi awe hana hatia.

Ikumbukwe wakati sakata hili linaripotiwa siku chache baadaye, msemaji huyo wa Yanga aliposti kuwa amekwenda nyumbani kwa Rais kuomba msamaha.

Hapa ndipo unapokuja ukweli alikuwa amemkosea. Binafsi nianze kulielezea suala hili kama ifuatavyo.

Hata kwenye ngazi ya familia tu, si ruhusa, au si vizuri kwa mdogo kumtolea maneno ya kashfa, dharau na vitisho mkubwa aliyekuzidi.

Hii tunafundishwa tu kwenye ngazi ya familia. hata kama mkubwa akikukosea kuna watu wa kwenda kuwaambia kuwa mzee fulani amenikosea, na wao ndiyo watakaomwita na kumuelezea kuletewa malalamiko na kijana, hivyo kumkanya mzee mwenzao.

Kama ukikosewa, halafu ukamshindilia na maneno mtu mzima ni wewe ndiyo utakayeonekana mkosefu.

Manara hakupaswa kumjia juu Karia kwa vyovyote vile kwani ukiachilia mbali cheo chake cha Rais wa TFF au Mwenyekiti wa Baraza la Soka Afrika Mashariki na Kati (CECAFA), lakini pia amemzidi umri.

Kiafrika si heshima wala adabu. Tukija kikazi Karia alikuwa kazini. Kosa limefanyika akiwa kwenye soka analoliongoza na wala mzozo huo haukufanyika barabarani au baa.

Ingekuwa ni ajabu kubwa kama Manara asingeadhibiwa, kwani alifanya hivyo mbele ya wageni rasmi uwanjani, wengine wakiwa na nyadhifa kubwa serikalini na kwenye chama.

Nakumbuka siku chache tu baada ya tukio hilo, Waziri wa Utamaduni, Sanaa na Michezo, Mohamed Mchengerwa alikumbusha wanamichezo na wadau kuwa na nidhamu katika michezo ili kuleta heshima pia kwa wachezaji wanaowaongoza.

"Nimepata taarifa kuna watu hawaheshimu viongozi wao. Niwaombe wachezaji, viongozi na wadau wote wa michezo kuzingatia nidhamu na maadili katika michezo," alisema waziri huyo.

Kokote kule kama hakuna nidhamu hakuna mafanikio. Manara si mtu wa kwanza kufungiwa baada ya kukiuka kanuni za uendeshaji. Wengi tu wameshafungiwa maisha, wengine miaka mitano, wakiwamo viongozi, wadau, wachezaji na makocha na wameendelea kutumikia vifungo vyao, baadhi hadi leo hii.

Nashangaa imekuwa taharuki kwa Manara, ambaye pia amekuwa na historia ya utovu wa nidhamu, ikumbukwe ni utawala wa Karia ndiyo uliomfungulia kwenye kifungo ilichokikuta kutoka kwenye utawala uliopita wa Jamal Malinzi, wakati huo akiwa Mkuu wa Kitengo cha Habari na Mawasiliano wa Simba.

Binafsi naunga mkono adhabu hii kwa sababu kama imefikia mpaka kumtolea maneno mabaya rais wa shirikisho, nani hapo baadaye ambaye angeweza kusalimika?

Huko mbele sasa angeweza kuzozana na mtu yoyote yule hata kwenye klabu yake.

Yanga na klabu zote zipo chini ya TFF, sasa kama kiongozi wa TFF inayoongoza soka lenyewe hajasalimika wa kwenye klabu yake watasalimika kweli? Nadhani wadau wa soka pia wana haki ya kuisadia TFF na siyo kuiyumbisha.

TFF ikiwapiga watu faini wanasema faini siyo dawa maana wana uwezo wa kulipa, ndiyo maana wanafanya makosa kila mara.

# Mwanza kujenga madarasa 11,000

Na Richard Makore, MWANZA

MKOA wa Mwanza umezindua mpango maalum utakaowezesha kujenga vyumba vya madarasa 11,000 katika wilaya zote ili kukabiliana na tatizo la wanafunzi kukosa sehemu ya kusomea.

Mpango huo uliopewa jina la "uzalendo kwanza kazi iendelee" utashirikisha wananchi, madiwani, wabunge pamoja na watendaji wa serikali katika wilaya zote za mkoa huo.

Mkuu wa Mkoa wa Mwanza, Robert Gabriel jana alikutana na watendaji mbalimbali wa wilaya na mkoa huo ili kujadiliana kwa kina kuhusu namna ya kuanza utekelezaji wa mpango.

Akizungumza katika kikao hicho, Gabriel alisema mpango huo utazinduliwa rasmi Julai 25, mwaka huu wilayani Misungwi mkoani Mwanza na kushirikisha wananchi katika hatua zote za ujenzi wa vyumba hivyo vya madarasa.

Aliongeza kuwa ni aibu kwa mkoa huo, kukabiliwa na uhaba wa vyumba vya madarasa wakati umejaaliwa kuwa na rasilimali za kutosha yakiwamo madini.

Gabriel alisema mahitaji ya mkoa mzima ni vyumba vya madarasa 18,000, lakini vilivyopo ni 7000 na kwamba kuna uhaba wa vyumba 11,000 mpaka sasa.

"Ukijua tatizo lako unakuwa umelitatua kwa asilimia 50 na hili ni lazima kila mdau ashiriki vyema ili kuhakikisha vyumba hivyo vinakamilika kama ilivyopangwa," alisema.

Vyumba hivyo vya madarasa 11,000 katika mkoa mzima ni kwa ajili ya shule za msingi na sekondari.

Akizungumza na watendaji wa serikali mkoani humo, Gabriel alisema mpango huo unalenga kushirikisha wananchi wa vijijini na wadau mbalimbali ili kuhakikisha wanakamilisha vyumba vyote 11,000 mkoani humo.

"Wananchi watasomba mawe, mchanga, kokoto na kushiriki kuchimba msingi, lengo hapa ni kuhakikisha tunajenga wenyewe kwa nguvu zetu pamoja na kushirikisha wadau," alisema

Aliwaagiza wakurugenzi wa halmashauri utakapozinduliwa ujenzi huo kuandaa bajeti kwa ajili ya kutengeneza uji wa maziwa ili watu wote watakaoshiriki kwenye ujenzi wanywe pamoja na wananchi huko vijijini wakati wakiendelea na kazi.

Gabriel alisema ni lazima mkoa ujitosheleze kwa vyumba vya madarasa pamoja na madawati ili kuhakikisha kila mwanafunzi anasomea ndani na kukalia dawati.

# Kenyatta akabidhi uenyekiti EAC kwa Rais Ndaishimiye

Na Cynthia Mwilolezi, ARUSHA

WAKUU wa nchi wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC) wamemchagua Rais wa Burundi, Evariste Ndaishimiye kuwa Mwenyekiti wa jumuiya hiyo kwa kipindi cha mwaka mmoja.

Akizungumza jana jijini Arusha mara baada ya kuchaguliwa katika mkutano wa 22 wa wakuu wa nchi wanachama wa EAC, Rais Ndaishimiye alishukuru viongozi wenzake kwa kumchagua kushika nafasi hiyo.

"Kipekee niwashukuru wananchi na Serikali ya Tanzania kwa mapokezi mazuri waliyotupatia katika nchi hii nzuri ya kuvutia," alisema.

Vilevile, alisema kuwa katika kipindi cha uongozi wake, ataongeza matumizi ya lugha ya Kiswahili katika jumuiya hiyo kama walivyokubalina kuwa Kishwahi kitakuwa lugha kuu ya maswasiliano.

Ndaishimiye aliahidi kutoa kipaumbele kwa wanawake na vijana katika masuala mbalimbali yanayohusu nchi za EAC.

"Nirudie kuwashukuru marais wenzangu kwa imani na ushirikiano mlionipa na kunichagua kushika nafasi hii," alisema. Pia alitumia fursa hiyo kumshukuru Rais Uhuru Kenyatta wa Kenya kwa mafanikio makubwa yaliyopatikana wakati wa kipindi chake cha uongozi.

Kenyatta alishukuru na kuaga rasmi Sekretarieti na EAC na baraza la mawaziri kwa ushirikiano alioupata katika kipindi cha uongozi wake na kufanikisha kupiga hatua ya maendeleo kwenye maeneo mbalimbali.

Alisema anachotamani kifanyike kwa haraka ni kupokewa kwa Somalia kuwa mwanachama wa EAC baada ya kuwasilisha ombi katika kipindi cha uongozi wake.

Alisema moja ya mafanikio aliyopiga katika kipindi chake kati ya Tanzania na Kenya, wameondoa vikwazo 52 kati ya 68 mpakani.

"Hii ni hatua kubwa tuliyopiga hadi kufikia hapa, ninaamini tutaendelea kupiga hatua zaidi ya hapa," alisema.

Akisoma maazimio ya Baraza la Mawaziri wa Nchi za EAC, mbele ya wakuu wa nchi hizo, alisema moja ya maazimio muhimu ni lugha ya Kiswahili kutumika rasmi kwenye shughuli zote za EAC.

Katika kikao hicho cha wakuu wa nchi wanachama, majaji wawili; Gavuko Leonard (Burundi) na Cheborion Barishoki (Uganda) waliapishwa kuwa majaji wa Mahakama ya Afrika Mashariki (EACJ).




Ofisa Udahili na Usajili wa Chuo cha Kodi (ITA), Pascal Gomba (wa pili kushoto), akifafanua jambo mbele ya wateja waliotembelea banda la Chuo hicho, katika Maonyesho ya 17 ya Vyuo Vikuu katika viwanja vya Mnazi Mmoja, jijini Dar es Salaam mapema wiki hii. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Uganda yakoshwa mradi gesi asilia

Na Zuena Msuya

UJUMBE kutoka Uganda umeipongeza Tanzania na kufurahishwa na utekelezaji wa mradi wa kuzalisha umeme kwa kutumia gesi asilia wa Kinyerezi jijini Dar es Salaam, baada ya kutembelea eneo hilo.

Katibu Mkuu Wizara ya Nishati, Mhandisi Felchesmi Mramba, alisema hayo juzi wakati wa ziara ya ujumbe huo uliohusisha Waziri wa Nchi anayeshughulikia Maendeleo ya Madini, Wizara ya Nishati na Madini ya Uganda, Mhandisi Peter Lokeris na Kamati ya Bunge ya Mazingira na Maliasili.

Ujumbe wa Uganda uko nchini kwa ziara ya siku sita kujifunza na kuona utekelezaji wa miradi mbalimbali ya sekta ya nishati kuanzia Julai 19 katika mikoa ya Dar es Salaam na Tanga.

Mramba alisema wageni hao wamefurahishwa na kazi kubwa ya uwekezaji iliyofanyika katika kutekeleza mradi wa Kinyerezi na kwamba wameipongeza serikali ya Tanzania kwa kutekeleza mradi huo adhimu kwa nchi za Afrika Mashariki.

Alisema ujio wao ni uthibitisho tosha kuwa nchi hizo mbili sasa ziko tayari kushirikiana katika rasilimali ya gesi asilia inayochimbwa nchini.

Mei, mwaka huu, Rais Samia Suluhu Hassan na mwenzake wa Uganda, Yoweri Museveni, walifanya mazungumzo juu ya ujenzi wa bomba la kusafirisha gesi asilia kutoka Tanzania hadi Uganda ili kuiwezesha nchi hiyo kuzalisha umeme unaotakana na gesi pamoja na matumizi mengine.

Viongozi hao walikubalina kuwa bomba hilo likijengwa lipite katika maeneo yenye watu ili gesi hiyo iendelee kutumika na baadaye lifike Uganda.

Waziri wa Nchi Lokeris na ujumbe alioambata nao, waliipongeza Tanzania kwa kutekeleza mradi mkubwa wa Kinyerezi ambao umesababisha nchi ya Tanzania kuwa na umeme mwingi na wa uhakika.

Alisema mradi huo pia umesababisha viwanda kuongezeka kwa wingi nchini humo kwa kuwa wawekezaji wanauhakika wa kufanya uzalishaji katika viwanda vyao muda wowote kutokana na kuwa na umeme na hiyo imechangia kasi kubwa ya ukuaji wa viwanda nchini humo.

Lokeris alifafanua kuwa Uganda inatamani kuwa na mradi kama huo nchini humo na kwamba baada ya kuona kilichofanyika, wataisisitiza serikali yao kuharakisha mchakato wa utekelezaji wa bomba la kusafirisha gesi asilia kutoka Tanzania hadi nchini mwao kwa kuwa wameshuhudia manufaa makubwa ya uwepo wa mradi huo Tanzania.

Mhandisi Lokeris alijinasibu kwa kusema endepo mradi huo utatekelezeka Uganda, nchi hiyo itakua kiuchumi kwa kuwa kutakuwa na uhakika wa kuwa na umeme mwingi na wa kutosha kuwezesha wawekezaji wengi kuwekeza nchini humo.

Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Mazingira na Maliasili wa Uganda, Emanuel Otara, alisema kamati hiyo imekuja kuangalia miundombinu ya gesi ambayo tayari viongozi wakuuu wa nchi hiyo wamezungumza na kuona namna ambavyo Tanzania imefanikiwa.

"Hakika tumefurahi sana kuona kuwa inawezakana mradi kama huo kufanyika Uganda na kuleta manufaa zaidi kwa taifa hilo kiuchumi. Baada ya kuona uwekezaji huo, wabunge tumeridhia mradi huo ufike Uganda na tumeelezwa kuwa mazugumzo yanaendelea vizuri juu ya utekelezaji wake, tuko tayari kuupokea," alisema.

# Wanaotaka kusoma nje waitiwa mikopo

Na Joseph Mwendapole

WAKALA wa Elimu Nje ya Nchi, Global Education Link (GEL), imewataka wanafunzi wanaotaka kwenda kusoma nje ya nchi lakini hawana uwezo kuchangamkia mikopo isiyo na riba inayotolewa na taasisi hiyo kwa kushirikiana na taasisi za fedha.

Ofisa Mikopo wa GEL, Musa Sultani, alisema hayo jana wakati wa maonyesho ya vyuo vikuu yanayoendelea kwenye viwanja vya Mnazi Mmoja, jijini Dar es Salaam.

Alisema mikopo hiyo inatolewa kuanzia kwa wanafunzi wanaotaka kwenda kusoma kuanzia ngazi ya cheti, stashahada, shahada ya kwanza, shahada ya uzamili na shahada ya uzamivu.

Sultani alisema GEL imekuwa ikishirikiana na benki ya Amana kutoa mikopo hiyo inayoanzia asilimia 50 mpaka 70 na ilianza kutolewa mwaka 2018 kupitia Benki ya Biashara ya Mwalimu.

Alisema mwaka 2018 walipokea maombi ya wanafunzi 150 lakini walionufaika kwa awamu hiyo ya kwanza walikuwa 80 na hakukuwa na mtu aliyeshindwa kulipa.

"Wote waliokopa walilipa mikopo hiyo na mwaka 2019/20 tulifanikiwa kutoa mikopo kwa wanafunzi 200 na wote walirejesha kwa wakati. Tunawakaribisha watu wanaotaka kusoma nje ya nchi lakini hawana fedha hizo waje GEL tutawapa," alisema.

Sultani alisema kama mwombaji ametimiza vigezo vyote kwa kuwa na nyaraka sahihi, anaweza kupata mkopo huo ndani ya saa 48.

Ofisa Uhusiano wa Benki ya Amana, Aziz Sangali, alisema benki hiyo imehudhuria maonyesho hayo chini ya mwamvuli wa GEL ili kuwaelezea wazazi kuhusu fursa hiyo ya mikopo isiyo na riba.

Alisema wanaohitaji mikopo ya aina hiyo wanafika GEL ambako hupewa utaratibu mzima wa kufuata zikiwemo nyaraka za kukamilisha ili kumwezesha kupata mkoo na ndipo taarifa zake zitawasilishwa Amana kwa ajili ya kulipwa.

"Mzazi anatakiwa kufika Global kushauriana na maofisa wake kuhusu kozi nan chi ambayo mtoto anataka kwenda kusoma, tunawakaribisha sana waje kupata mikopo," alisema Sangali.

Alisema wazazi wengi wamekuwa wakichukua mikopo isiyozidi milioni 25 na asilimia 100 ya wakopaji hao wamekuwa wakirejesha bila usumbufu wowote.

Sangali alisema mzazi au mlezi anayechukua mkopo huo anapewa miezi nane kulipa na wamekuwa wakiruhusiwa kulipa kwa awamu .

"Mkopo huu utakatiwa bima ya maisha hivyo mtu atakayeuchukua na kupata ulemavu au kufariki dunia basi bima italipa mkopo wake," alisema Sangali.



Katibu Mkuu Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia, Dk. Francis Michael akizungumza na watumishi wa Mamlaka ya Elimu Tanzania (TEA), katika Makao Makuu ya TEA, Mikocheni, Dar es Salaam ikiwa ni sehemu ya ziara ya kutembelea taasisi zilizo chini ya wizara yake, kwa lengo la kuangalia zinavyotekeleza majukumu yake. Kushoto ni Mkurugenzi Mkuu wa TEA, Bahati Geuzye. **PICHA: JOSEPH MWENDAPOLE**

## Mkutano waitishwa kujadili ubora elimu

Na Elizabeth Zaya

MTANDAO wa Elimu Tanzania (TEN/MET) umeandaa mkutano wa kimataifa wa kujadili mustakabali wa elimu ndani na nje ya Tanzania.

Mratibu wa Taifa wa mtandao huo, Ochola Wayoga, alisema jana jijini Dar es Salaam kuwa mkutano huo utatoa fursa kwa wadau wa elimu wakiwamo maofisa wa serikali, watunga sera, vyuo vikuu, wanafunzi, watafiti, taasisi za elimu, mashirika ya umma na binafsi na mashirika ya maendeleo, kujadili hali ya ubora wa elimu.

Alisema mkutano huo unatarajiwa kufanyika Agosti 17 hadi 19, mwaka huu, na lengo kubwa ni kuboresha utoaji wa elimu nchini na kwamba mada kuu itakuwa kutafakari upya nafasi ya elimu katika kuleta mabadiliko endelevu duniani.

"Mkutano huu wa pili kimataifa wa elimu bora, unaandaliwa na TEN/MET ili kutoa fursa kwa wadau wa elimu ná wajumbe kote Afrika na ulimwenguni kubadilishana uzoefu na maarifa yao kwa dhumuni la kuboresha elimu," alisema Wayoga.

"Mkutano huo pia utatumika kusambaza matokeo ya utafiti kuhusu tafiti mbalimbali za elimu, kubadilishana uzoefu kuhusu mbinu za ugharimiaji wa elimu, mitizamo ya kimataifa na ya ndani na kushawishi mabadiliko ya sera ya elimu katika mwelekeo sahihi kwenye karne ya 21," aliongeza

Wayoga alisema wanatarajia kwamba mkutano huo utasaidia kubuni na kutoa maamuzi kuhusu mbinu bunifu za kuboresha elimu, kupata uzoefu wa teknolojia na utaalamu kuhusu usimamizi bora katika sekta hiyo, pamoja na kupata suluhu za kushughulikia ubora na umuhimu wa sekta hiyo. "Na jopo la majadiliano litaangazia pia lugha za kiafrika katika kufundishia, kufikiria upya mustakabali wa pamoja wa mkataba mpya wa kijamii wa elimu, kuboresha teknolojia ya kufundishia na kujifunzia ili kupunguza pengo la kidijitali katika sekta hiyo.

"Litaangazia namna ya kuchukua hatua za haraka za kupunguza athari mbaya za UVIKO-19 kwa watoto na vijana, namna ya kuimarisha mfumo wa data ya elimu nyakati za dharura na migogoro, uboreshaji wa sera ya elimu, mitaala na stadi za kazi," alisema.

Alitaja miongoni mwa nchi ambazo zimethibitisha kushiriki kuwa ni Kenya, Msumbiji, Zambia, Zimbabwe, Uganda, Somalia, Sudani na Marekani.

## Familia yapinga kiapo kinzani cha uchunguzi ndugu kufia mahabusu

Na Grace Gurisha

FAMILIA ya Stella Moses, aliyefia mahabusu, imepinga kiapo kinzani cha Mkuu wa Jeshi la Polisi na wenzake katika shauri la maombi ya uchunguzi wa kifo hicho kwa madai kimewasilishwa mahakamani kinyume cha sheria.

Mbali na IGP, wajibu maombi wengine katika shauri hilo ni Kamanda wa Polisi Kanda Maalum Dar es Salaam (ZPC) na Kamanda wa Polis Mkoa (RPC) wa Kipolisi Kinondoni.

Wengine ni Mkuu wa Polisi Wilaya (OCD) ya Kipolisi Mburahati, Mkurugenzi Mtendaji wa Hospitali ya Taifa Muhimbili na Mwanasheria Mkuu wa Serikali.

Pingamizi hilo la familia liliwasilishwa juzi na wakili wao, Peter Madeleka, mbele ya Hakimu Mkazi, Aaron Lyamuya wa Mahakama ya Hakimu Mkazi mkoa wa Dar es Salaam Kivukoni (Kinondoni).

Madeleka alidai kwamba nakala ya kiapo kinzani walichopewa hakionyeshi kama kimewasilishwa mahakamani kwa mujibu wa sheria, kwa hiyo kiapo hicho cha pamoja cha wajibu maombi kimewasilishwa isivyo sahihi.

Wakili huyo, aliiomba mahakama hiyo ione kwamba hakuna kiapo kinzani cha wajibu maombi na kisha ipange tarehe ya usikilizwaji wa maombi hayo.

Akijibu hoja hizo, Wakili wa Serikali, Daisy Makakala alidai kuwa nakala aliyo nayo Madeleka ameiomba tu akampatia, lakini waliyoiwasilisha mahakamani imefuata utaratibu zote za mahakama.

Baada ya majibu hayo, Hakimu Lyamuya aliuliza nakala waliiwasilisha lini, ambapo Makakala akajibu kuwa Julai 11, mwaka huu.

"Baada ya kuwasilisha mahakamani nyaraka hii, tulimtumia Madeleka kwa baruapepe. Kwa hiyo naomba mahakama ichukue kuwa majibu ya wajibu maombi yamefika mbele ya mahakama kwa wakati," alidai Makakala.

Baada ya Makakala kudai hayo, Madeleka alidai nyaraka waliyopaswa kupewa ni ile iliyowasilishwa mahakamani na kuwa sehemu ya kumbukumbu za mahakama na kwamba anaamini kuwa aliyopewa ndiyo iliyoko mahakamani.

Hakimu Lyamuya baada ya kusikiliza hoja za pande zote, aliahirisha shauri hilo hadi Agosti 2, mwaka huu, kwa ajili ya uamuzi.

Stella alifariki katika mahabusu ya Kituo cha Polisi Mburahati, Desemba 20, 2020. Aljisalimisha baada ya kupata taarifa kuwa alikuwa anahitajika na polisi walidai kuwa alijinyonga huku ndugu zake wakipinga kwa madai kwamba kuna utata wa kifo hicho.

Machi, 2022 familia kupitia shemeji wa marehemu, Emmanuel Kagongo, ilifungua shauri la maombi katika Mahakama ya Hakimu Mkazi Kivukoni kuomba iamuru ufanyike uchunguzi huru kujua ukweli wa mazingira ya kifo hicho.

Kwa mujibu wa hati ya kiapo chake, Kagongo anadai kuwa Desemba 28, 2020 Idara ya Vizazi na Vifo katika Hospitali ya Taifa Muhimbili ilitoa kibali cha mazishi kwa Eliud Kagongo kuridhia mazishi ya mwili wa marehemu Stella huku kibali kikiwa hakikuonyesha sababu za kifo chake.





## Maandalizi Nanenane Kanda ya Kati yaiva

**Na Ibrahim Joseph,** DODOMA

MAANDALIZI ya uwanja wa maonesho ya sikukuu ya wakulima (Nanenane) Kanda ya Kati yanayotarajiwa kuanza Agosti Mosi, mwaka huu, yanaendelea vizuri.

Mjumbe wa Kamati ya Maandalizi hayo Kanda ya Kati, Mhandisi David Chitemo, alisema hayo alipozungumza na Nipashe kwenye eneo la uwanja huo, Nzunguni jijini hapa jana.

Mhandisi Chitemo alisema maandalizi hayo ya sikukuu hiyo ya nanenane kwa Kanda ya Kati yanaendelea vizuri na wanategemea kuanza kwa wakati maalumu waliokusudiwa.

Alibainisha kuwa maonyesho hayo yanashirikisha wananchi wa Mikoa ya Singida na Dodoma chini ya mwenyekiti wake, Mkuu wa Mkoa wa Dodoma, Anthony Mtaka na mwenyekiti mweza Mkuu wa Mkoa wa Singida, Dk. Binilith Mahenge.

Chitemo alizitaka kazi za maandalizi zinazoendelea katika viwanja hivyo kuwa ni ujenzi wa miundombinu ya barabara pamoja na kuboresha miundombinu ya umeme kwenye mabanda.

Mhandisi Chitemo alizitaja kazi zingine zinazoendelea kuwa ni kuboresha uzio wa uwanja huo ili kudhibiti upotevu wa mapato ya viingilio na kutakuwa na ujenzi wa mabanda kwa jailli ya wadau watakaoshiriki.

Alisema mwaka huu wanatarajia kuwa zaidi ya taasisi za umma 50 na zaidi ya kampuni 60 kushiriki maonyesho hayo .

Pia alisema Halmashauri zote za mikoa hiyo miwili zitashiriki maonyesho hayo pamoja na wafanyabiashara za chakula na wachuuzi wa bidhaa mbalimbali na wajasiliamali zaidi ya 1,000 watashiriki.

Alitaja makundi mengine yatakayoshiriki kuwa ni wizara za serikali na taasisi zake kwa sababu ya uwapo wa makao makuu jijini hapa hapa, hivyo zimekaribishwa kushiriki.

Pia alisema katika maenyesho hayo kutakuwa na viingilio ambayo vitatozwa kwa kampuni na taasisi zitakazoshiriki.

Alisema kwa wafanyabiashara wadogo kama mama lishe na baba lishe, nao watakuwa na viwango tofauti vya kulipa ushiriki wa maonyesho hayo.

Aliyataja mapato mengine yatakayokusanywa kupitia maonesho hayo ni ushuru wa magari yatakayokuwa yakiingizwa kwenye viwanja hivyo na wananchi watakaotembelea maonesho hayo watachangia.

Maonesho hayo ya Sikukuu ya Wakulima kwa mwaka huu kitaifa, yanatarajiwa kufanyika Mbeya kwa kushirikisha mikoa yote ya Tanzania Bara na Visiwani.

# Waliofanya udanganyifu ardhi kikaangoni

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

MKUU wa Mkoa wa Dodoma, Anthony Mtaka, amewataka wananchi waliofanya udanganyifu wa kujiandikisha katika orodha ya watu wanaodai fidia ya maeneo yao, kujisalimisha huku akiwapa siku saba kujiondoa kwenye mpango huo.

Mtaka alitoa agizo hilo jana jijini hapa wakati akizungumza na viongozi wa mkoa na watumishi wa idara ya ardhi kuhusu tamko la madai ya viwanja vya eneo la Msalato.

Alisema pamekuwapo na madai ya baadhi ya wananchi kwamba wana uhalali wa kudai fidia kwa maeneo yasiyowahusu wakati hawana umiliki.

"Kuna baadhi ya wananchi baada ya kuona kuna uongozi mpya wamekuwa wakileta udanganyifu kuwa wananchi waliopewa hati si wamiliki halali, hivyo nitoe wito wajisalimishe mara moja," alisema Mtaka

Pia alitoa rai kwa wananchi wenye viwanja kuacha udalali wa viwanja visivyo wahusu huku akisisitiza kuzingatia sheria za ardhi wakati wa ujenzi.

Katibu Tawala wa Mkoa wa Dodoma, Dk. Fatma Mganga, alitoa wito kwa wananchi na viongozi wote kuacha udanganyifu na kuzalisha migogoro isiyo ya lazima na kuwa na hofu ya Mungu kwa kutenda haki.

Katibu Tawala Msaidizi anayeshughulikia Miundombinu, Mhandisi Happiness Mgalula, alisema suala la ulipaji wa fidia eneo la Msalato lilifanyika mwaka 2008, 2012 na 2019 huku akibainisha kuwa kuna wengine wamekuwa na tabia ya kubadilisha majina.

"Kama wewe ulikuwa mtoto amelipwa mzazi wako halafu unakuja kudai kulipwa, hilo haliwezekani. Msako utafanyika kwa wale wanaofanya udanganyifu," alisema.

Mkuu wa Wilaya ya Dodoma, Jabir Shekimweri, alisema ili kujiepusha na migogoro ni vyema wananchi kujiridhisha kabla ya kununua maeneo kwa watu binafsi na kwamba ofisi ya wilaya imekuwa ikichukua hatua kwa watumishi wasio waaminifu.

Shekimweri alisisitiza kuwa kiwango cha teknolojia ya habari na mawasiliano (TEHAMA) katika ugawaji wa ardhi kinapaswa kutumika ili kuepusha migogoro.

Mhandisi wa Mradi wa Wakala wa Barabara (TANROAD) Mkoa wa Dodoma, Mhandisi Colman Ramadhan, alisema wananchi 1,919 wameshalipwa fidia ya jumla ya Sh. bilioni 14.99 katika uwanja wa ndege Msalato huku barabara ya mzunguko (Ring Road) wakilipwa wananchi 2,808 Sh. bilioni 16.25.




Mjumbe wa Kamati ya maandalizi ya maonyesho ya Nanenane, Kanda ya Kati, Mhandisi David Chitemo (kulia), akisimamia ujenzi wa miundombinu ya barabara kwenye Uwanja wa maonyesho wa Nanenane Nzuguni, jijini Dodoma juzi, ikiwa ni maandalizi ya sikukuu wakulima ya Nanenane kwa kanda hiyo, inayotarajiwa kuanza Julai 30 mwaka huu. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

## Mkakati kabambe kuongeza uzalishaji pamba

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

SERIKALI imeweka mkakati kuhakikisha wakulima wa pamba nchini wanakuwa na uwezo wa kuzalisha tani milioni moja ifikapo 2025 kwa lengo la kuwawezesha kujiinua kiuchumi.

Hayo yalibainishwa na Mkurugenzi Mkuu wa Bodi Pamba Tanzania (TCB), Marko Mtunga, wakati akizungumza na waandishi wa habari kuhusu kuongeza uzalishaji wa zao hilo katika maeneo mbalimbali nchini.

Mtunga alisema moja ya mikakati ambayo imewekwa ili kufikia lengo hilo ni pamoja na kuwapatia wakulima mbegu bora ambazo zitawasaidia kupata mazao kwa kwa wingi wakati wa mavuno.

"Tumejipanga kushirikiana na Wakala wa Mbegu nchini ili kuhakikisha mbegu bora za zinapatikana na kuwafikia wakulima kwa wakati"alisema Mtunga. Pia alisema ufadhili uliotolewa na serikali ya Brazil kwa kushirikiana na serikali ya Tanzania kwenye kilimo cha pamba utachangia kuchangia ukuaji wa kilimo hicho katika mikoa ambayo zao hilo linastawi.

Alisema mwaka huu uzalishaji haukuwa mzuri kutokana na mabadiliko ya tabia nchi na kuongeza msimu ujao, serikali imejipanga kuhakikisha wanafika mbali katika kilimo hicho cha zao la biashara.

Hata hivyo, alisema msimu ujao uzalishaji unaweza kuwa mkubwa kutokana na mikakati ambayo imewekwa ili kuhakikisha zao hilo linakuwa kwa kasi.

Mkurugenzi huyo aliishkuru serikali kutokana na kujikita zaidi kwenye kilimo ikiwamo kuwekeza kwenye zao hilo ili kuwainua wakulima, hivyo akaihakikishia serikali kuwa wakulika hawataiangusha.

Mkulima Joseph Maganga alisema zao hilo ni tegemeo katika Kanda ya Ziwa, hivyo serikali imefanya jambo kuwekeza kwenye kilimo hicho ambacho kitawasaidia wakulima kupiga hatua kiuchumi.

Alisema zao hilo lilishasahaulika kwa muda mrefu, hivyo uwekezaji huo utazidi kuwahamasisha wakulima kuingia kwenye kilimo hicho.



HABARI ZANZIBAR

# Mwinyi awapa kibarua viongozi wilaya, mkoa

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

RAIS wa Zanzibar Dk. Hussein Ali Mwinyi, ameutaka uongozi wa wilaya na mkoa wa Kaskazini Unguja kushirikiana na kuhakikisha wananchi wanapata zana, vifaa, vya elimu na mitaji ili kufanikisha dhana ya uchumi wa bluu, hususan kupitia sekta ya uvuvi.

Dk. Mwinyi amesema hayo jana katika Hoteli ya Melia, Kiwengwa mkoa wa Kaskazini Unguja katika hafla ya majumuisho ya ziara yake ya kutembelea na kukagua miradi mbalimbali ya maendeleo katika mkoa huo, inayotekelezwa kupitia fedha za ahueni ya UVIKO - 19 na miradi mingineyo.

Alisema kuna umuhimu kwa viongozi hao kushirikiana kwa kuwapatia mambo hayo ili kufanikisha kikamilifu dhana ya uchumi wa bluu, kupitia sekta za utalii, uvuvi, kilimo hasa cha mwani, fukwe na rasilimali zingine za bahari.

Uchumi wa bluu, alisema ni eneo ambalo serikali imelipa kipaumbele huku akibainisha azma iliyopo ya kujenga Bandari kubwa ya kisasa katika eneo la Mangapwani kuwa inalenga kuibua ajira na kuimarisha uchumi.

Aidha Dk. Mwinyi aliyataka mabaraza ya miji kuhakikisha yanaleta maendeleo kwa wananchi kwa kutumia fedha yanazokusanya kwa ajili ya miradi ya mendeleo.

Alieleza kufurahishwa na hali ya ulinzi na usalama katika mkoa huo ilivyo na kubainisha kuwa amani ndiyo mtaji wa kwanza wa nchi, hivyo kuna haja ya kudhibiti uhalifu, hususan kwa watalii.

Kuhusu kisiwa cha Tumbatu, Dk. Mwinyi aliwataka mawaziri wa sekta za maji, elimu, afya, ujasiriamali na uwekezaji kushirikiana ili kutimiza ahadi mbalimbali alizoweka kwa wananchi.

Alisema kuna umuhimu wa kushirikiana ili kusaidia maendeleo ya kisiwa hicho, kutokana na mazingira kilivyo, huku akibainisha baadhi ya ahadi hizo kuwa ni pamoja na ujenzi wa hospitali ya wilaya ndogo ya Tumbatu, ujenzi wa gati, shule ya ghorofa , kiwanja cha mpira na kukamalisha ujenzi wa tangi la maji.

Katika hafla hiyo, Dk. Mwinyi alipata fursa ya kuelezea utekelezaji wa miradi katika sekta mbalimbali zikiwamo afya, elimu, ujasiriamali na uwezeshaji wananchi kiuchumi, ambazo zinatekelezwa kupitia fedha za ahueni za UVIKO - 19 na kusema ameridhishwa na utekelzaji sambamba na kukipongeza kikosi cha mafunzo kwa kazi nzuri na yenye kiwango.

Rais Dk. Mwinyi alizindua madarasa manane katika Shule ya Msingi Mahonda na kusema Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali itatenga fedha maalumu kwa ajili ya kuyafanyia ukarabati madarasa makongwe nchini kote.

Aidha, Dk. Mwinyi alifika katika Bonde la Mpunga Upenja na kupata taarifa ya maendeleo ya Mradi wa Miundombinu ya Umwagiliaji maji na kumshukuru Mkandarasi wa Mradi huo kwa kuwa muungwana na kukubali kuzifanyia marekebisha kasoro zilizojitokeza katika utekelezaji wa mradi kwa kutumia fedha zake mwenyewe.

Aliitaka Wizara ya Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo kusimamia vyema ugawaji wa vitalu katika Bonde hilo kwa kuwashirikisha wakulima, huku akiwahadharisha watendaji wa Serikali kutojihusisha na umiliki wa maeneo yanayogawiwa.




Naibu Waziri wa Afya Zanzibar, Hassan Hafidh, akizungumza na masheha na madaktari wa Wilaya ya Magharibi A'na B' Unguja, kuhusu umuhimu wa chanjo ya UVIKO-19, wakati wa uzinduzi wa kampeni kuhamasisha chanjo hiyo, katika Hospitali ya Kianga, Wilaya ya Magharibi "A" Mkoa wa Mjini Magharibi Unguja jana. **PICHA: RAHMA SULEIMAN**

# SMZ kuweka kipaumbele wanawake kushiriki uhandisi na ufundi umeme

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

KATIBU Mkuu Kiongozi, Mhandisi Zena Ahmed Said, amesema serikali itatoa kipaumbele kwa wanawake katika kila wizara kushiriki kazi za uhandisi, ufundi umeme, na kazi zingine ili kuweka usawa kwa wanawake wenye sifa.

Alisema kuna kuangalia usawa kwa sekta zote nchini pamoja na kuacha mfumo dume uliopo na kwamba endapo mwanamke amekidhi vigezo, apewe nafasi ya ajira kwenye sekta hizo ambazo wanaume ni wengi kuliko wanawake.

Mhandisi Zena aliyasema hayo wakati akizungumza katika warsha ya mradi wa mabadiliko ya sekta ya nishati Zanzibar, wadau mbalimbali kutoka Wizara ya Maji, Nishati na Madini.

Mradi huo unalenga kutoa uelewa wa kuwahamasisha wanawake kutumia fursa za kitaalamu ili kuleta mabadiliko sawa kwa wote. Alisema kuwapo kwa mradi wa mabadiliko ya sekta ya nishati Zanzibar, kutasaidia kwa kiasi kikubwa kuongeza idadi ya wataalamu wanawake katika sekta hiyo.

Katibu Mkuu Kiongozi alisema utafiti unaonyesha kuwa bado kuna idadi ndogo ya matumizi ya nishati kwa wanawake kutokana na mitazamo iliyojengeka ndani ya jamii kuwa sekta hiyo ipo kwa ajili ya wanaume.

Mhandisi Zena alibainisha kuwa kwa sasa serikali imeona kuna umuhimu wa kufanyia kazi kasoro hizo ili kuona sekta zote zinakuwa na usawa wa kijinsia.

Pia aliiomba jamii kujikita zaidi katika malezi ya usawa wa kijinsia ili kuwajengea misingi bora.

Naye Katibu Mkuu Wizara ya Maji, Nishati na Madini, Josseph Kilangi, alisema atahakikisha kupitia wizara yake kuona wanawake wanakuwa mstari wa mbele katika mradi huo hususani wa masomo ya sayansi ikiwamo fani ya uhandisi.

Alisema lengo ni kutoa uelewa juu ya kutambua kuwa wanawake nao ni sehemu ya kufanya kazi hizo ikiwemo ufundi umeme na uhandisi wa sekta tofauti za kisayansi kutokana na serikali kuthamini uwapo wao.

Kilango alisema kila mwananchi ana haki ya kufanya kazi kama ana vigezo vinavyohitajika na sehemu husika na si kukandamizwa kutokana na jinsia yake.

# Masheha watakiwa kuhamasisha chanjo

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

MASHEHA na madaktari katika wilaya za Magharibi A na B Unguja, wametakiwa kuhamasisha wananchi kushiriki katika chanjo ya UVIKO -19 ili kujikinga na maradhi hayo.

Akizungumza katika uzinduzi wa kuhamasisha chanjo hiyo katika Uwanja wa Hospitali ya Kianga, Naibu Waziri wa Afya, Hassan Hafidh, alisema takwimu zinaonyesha wilaya hizo hazijahamasika katika chanjo hiyo, jambo ambalo linarudisha nyuma juhudi za serikali katika mapambano hayo .

Alisema serikali za mitaa kwa kushirikiana na wafanyakazi wa sekta ya afya katika shehia zao (afya ya jamii) zinapaswa kupita kila sehemu na kila nyumba kuhamasisha jamii ili kuchanja.

Pia alibainisha kuwa wizara kwa kushirikiana na wadau wa maendeleo ina jukumu la kuhakikisha wanalinda na kuwakinga wananchi wao kutokana na maradhi mbalimbali kwa kutafuta dawa za kupambana na maradhi ikiwamo chanjo ya UVIKO- 19 ili Zanzibar ibaki salama.

"Lazima tuhakikishe tunawalinda na kuwakinga wananchi wetu katika kupambana na maradhi ya UVIKO -19. Haya ni maradhi hatari na yanasambaa kwa kasi zaidi, hivyo tujitokeze tukachanje ili tujikinge," alisema.

Naibu Waziri aliwataka wananchi wa wilaya hizo kujitokeza kwa wingi kupata chanjo hiyo, kwa sababu wanaopata maambukizi ni wale ambao hawajapata chanjo na kinga ni bora kuliko tiba.

Naye Mratibu wa Chanjo hiyo, Abdulhamid Ameir Saleh, alisema Magharibi A na B ni miongoni mwa wilaya sita ambazo hazikufanya vizuri katika chanjo hiyo jambo ambalo linahatarisha maisha ya wananchi.

Alisema kuwa kutokana na hali hiyo kuna mikakati maalumu ya kuhamasisha wananchi kujikinga na endapo watajitokeza kuchanja itasaidia kasi ya maambukizi kupungua.

Mwakilishi kutoka Shirika la Afya Duniani (WHO), Dk Andamichel Ghirmay, aliishukuru Wizara ya Afya kwa kuamua kufanya uzinduzi huo katika wilaya hizo na kuendeleza mashirikiano yaliyopo katika sekta ya afya.

Nipashe

MWANGA WA JAMII

BT BURUDANI TELE

JUMAMOSI JULAI 23, 2022




# NENDA FARIDA SABU

## Umemaliza kazi, mengi watayaenzi

JINAMIZI la kuwapoteza waigizaji wakongwe linazidi kutikisa, baada ya msanii mwingine wa filamu Farida Sabu, maarufu kama Mama Sonia, kufariki dunia juzi.

Siku chache zilizopita tasnia hiyo ya filamu ilimpoteza msanii mwingine mkongwe Bi Mwenda.

Mashabiki wa filamu za Bongo Muvi, watakosa kumuona tena tabasamu pana la Mama Sonia, ambaye wengi walipenda jinsi alivyokuwa akiigiza kama mama.

Kipaji chake kilianza kuonekna wakati akiwa katika kundi la Kaole Sanaa Group na kuigiza kwenye maigizo kama Dira, Gharika na Taswira.

Imeelezwa kwamba Farida alifariki Zanzibar alipokwenda kwa ajili ya kuitembelea familia yake na huko aliugua na kufariki juzi.

Wasanii mbalimbali wanazidi kutoa vilio vyao kwa kutuma salamu za rambirambi kwa familia na wanatasnia kwa ujumla.

Mwenyekiti wa Chama cha Waigizaji Chiki Mchoma,amesema msiba huo umeshtusha na kwamba hakuamini pale alipopata taarifa ya kufariki kwake.

"Bi Farida Bibi Sonia amefariki Zanzibar Unguja, mwezi mmoja uliopita alikwenda kwa ajili ya kupumzika na Watoto wake lakini akapatwa na maradhi na leo asubuhi Mungu akamchukua" alisema kwa masikitiko," Mchoma.

BASI SAWA

## Hennesseyy kuileta 'The Beginning' Agosti 5



MKALI wa Bongo Fleva, Hennesseyy, amekamilisha mipango ya kuachia albamu yake inayoitwa 'The Beginning' itakayotoka mapema mwezi ujao.

Akizungumza na BT jana, Hennesseyy, amesema ndani ya The Beginning, mashabiki watapata ladha ya ngoma tofauti tofauti hivyo wakae tayari kuipokea itakapotoka Agosti 5, mwaka huu.

"Kila kitu kimekamilika nasubiri tarehe ifike ili niweze kutoa albamu hii ambayo italeta mapinduzi kwenye muziki wetu, nimejitahidi kuwapa ladha mbalimbali mashabiki naamini wataifurahia na ninaomba waendelee kunipa sapoti pindi nitakapoiachia kwenye mitandao yote ya kuuza na kusikiliza muziki," amesema Hennesseyy ambaye ni bosi wa lebo ya Spacious Music.

## Dj Joozey kumpamba Khaleed



DJ kutoka Bongo, Joseph Misa 'DJ Joozey', amekuwa muwakilishi pekee kutoka Afrika Mashariki katika albamu ya God Did ya mwanamuziki maarufu duniani kutoka Marekani DJ Khaleed.

Akizungumza na BT, DJ Joozey amesema baada ya kuwa mmoja wa watu waliotumika kutangaza albamu ya DJ Khaled, anajivunia kutangaza nchi yake.

"Hii hatua kwangu ni kubwa sana ya kuonwa ninafaa kuitangaza albamu hiyo ya DJ mkubwa duniani ambaye ni mmoja wa mtu walionishawishi kuingia kwenye kazi ya kuburudisha, ninafanya hivyo kuitangaza lugha yangu adhimu ya Kiswahili," amesema DJ Joozey.



# SERIKALI YAAGIZA MIKOA KUPOKEA MAONI

NAIBU Waziri wa Utamaduni, Sanaa na Michezo Pauline Gekul amewaagiza maofisa utamaduni kote nchini katika mikoa, wilaya na halmashauri kukaa na wasanii katika maeneo yao ili kuchukua maoni yao yatakayoiwezesha serikali kuweka mifumo itakayowasaidia kunufaika na kazi zao.

Alitoa maelekezo hayo katikati ya wiki hii alipokutana na wasanii kutoka Arusha, Kilimanjaro na Tanga ambao walishiriki katika kikao cha kamati ya kuratibu na kusimamia hakimiliki.

Gekul, amesema serikali kupitia Mfuko wa Utamaduni na Sanaa kwa mwaka wa fedha 2022/23 imetenga Sh. Bilioni mbili ambazo moja ya majukumu yake ni kutoa elimu kwa wasanii inayoendana na maadili ya kitanzania.

"Wasanii ndio mnafahamu nini kiboreshwe zaidi, sisi serikali tunapokea maoni yenu na tutayafanyia kazi, nimewaomba wajumbe wa kamati wawe wavumilivu, wapokee maoni ya yale yasiyo ya mirabaha watuletee kwa sababu tumeamua kuondoa malalamiko kwenye sekta hii ya sanaa," alisema.





# Baba Levo uchawa hadi kwa Rayvanny?

MWANAMUZIKI asiyeishiwa na maneno, Baba Levo amesema Rayvanny, baada ya kuondoka Wasafi, anatarajiwa kuachia ngoma yake akishirikiana na msanii mkubwa.

Baba Levo amesema katika kibao hicho Rayvanny anaimba na mwanamuziki Luanav Jollea.

Hata hivyo, Rayvanny alikiri ujio wa ngoma hiyo na alimwagia sifa Baba Levo na kumuita mshua wake.

# Igumba: Kijiji cha Wasiojulikana

**Na Adam Fungamwango**

LEO tunaiangalia filamu iitwayo 'Igumba'. Imechezwa na wasanii Amri Athumani maarufu kama mzee Majuto, Amiri Simba, Sabrina Francis, Hashim Kambi, Mark Mfugale, Emmanuel Mtega, Shaaban Hassan na wengineo.

Inazungumzia kisa cha waigizaji ambao walilazimika kuigiza filamu kwenye kijiji hicho baada ya kutokea matatizo, lakini kilichowatokea haikuwa cha kawaida.

Jacky, na wengine zaidi ya 15, walitoka jijiji Dar es Salaam kwenda Dodoma kuigiza kwa ajili ya kutengeneza filamu kabambe. Lengo lao ifanye vema kwenye soko ili wajipatie kipato.

Wanafika kwenye pori moja mkoani Dodoma, dereva anatoka kwenda kujisaidia, lakini harudi.

Baada ya baadhi ya wasanii kuingia ndani kidogo porini wanarejea na viatu alivyokuwa amevaa, mwenyewe hajapatikana.

Wasanii wanaamua kuingia ndani kidogo ya pori hilo, na kukuta sehemu moja nzuri ambayo wanaweza kuigiza filamu yao kama kule ambako walitarajia kwenda.

Mmoja wa viongozi wa kijiji hicho, Hashim Kambi anapata habari kuwa kimeingiliwa na wageni ambao haijulikani wametoka wapi.

Anawaambia wanakijiji kuwa jambo hilo halipaswi kudharauliwa kwa sababu haijulikani wana nia gani.

Mzee wa kijiji, mzee Konde anawafuata akiwa na walinzi na kuwaambia waondoke mara moja kwa sababu wameingia bila ruhusa, lakini pia wamevunja mila na desturi za kijiji hicho.

Wasanii hao wanatoa hoja zao kuwa wameingia pale kwa bahati mbaya baada ya dereva wao kupotea, hivyo gari halina dereva na wameamua kufanya 'shooting' kwenye kijiji kile kile, pia hawajavunja sheria yoyote.

Kumbe Igumba ni kijiji ambacho tayari kilikuwa kimeshavunja mila na desturi zake, hivyo mikosi ilianza kukiandama.

Himaya nyingine ilianza kukishambulia kijiji hicho. Ikaita vijana wote ili kupigana na kukitetea kijiji hicho.

Wakati huo huo, kitu kisichojuliana kikiwa porini kilianza kuwashambulia na kuwaua watu kwenye kijiji hicho ikiwemo mpaka wale wasanii.

Wapo waliokufa kwa kukutana au kukutwa na watu wanaopigana vita, lakini wapo waliokuwa wanakufa katika mazingira tata kama alivyopotea dereva wao.

Ikawa ni mshikemshike kijijini hapo, wasanii wao ikawa ni kukimbia kila mmoja kuponyesha roho yake. Pamoja na kusaidiana, lakini pia walikuwa wakilaumiana na kukubali kupiga kambi hapo.

Mwisho wa siku hata viongozi wa kijiji hicho walikufa katika mazingira ambayo ilionyesha mizimu imekasirika.

Kijana Jacky na mpenzi wake ndiyo waliobaki hai kati ya wale wasanii zaidi ya 15 walioingia kwenye msitu wa kijiji cha Igumba.

Hawakuamini macho yao walipofanikiwa kujitosa mtoni, kuogelea na kuvuka ng'ambo ya pili, wakiwa salama salimini.

## BONGOFLEVA WANAOTUMIA MAJINA HALISI

**Na Adam Fungamwango**

KARIBU asilimia 70 mpaka 80 ya wasanii wengi wa muziki duniani hujulikana kwa majina yao maarufu ya kisanii na wala si yale halisi.

Wasanii wengi duniani hutumia majina ya kutungwa na mashabiki au kujitungia wenyewe, yakiwa ama yanalingana na kile kitu wanachokifanya, au kifupi cha majina yao.

Lengo ni kufanya majina yao kutamkika vizuri, tofauti na baadhi ya majina halisi ambayo mengine ni marefu ya hayaonekani kuwa na mvuto mbele ya wanaoyasikia.

Kumekuwa na mlolongo wa wasanii wengi kuwa na majina yao maarufu ambayo si yao halisi, kiasi cha majina yao halisi yasijulikane kwa mashabiki.

Hata hivyo, wapo wasanii wachache hawakutaka kubadilisha majina na pia waliona ustaa unatengenezwa na msanii mwenyewe pamoja na ngoma zake na wala si jina.

**Ali Kiba**

Ni msanii staa zaidi nchini Tanzania ambaye anatumia jina lake halisi. Ni nembo ya muziki wa bongo fleva Tanzania aliyeingia kwenye fani hii mwanzoni mwa miaka ya 2000.

Kiba ameingia kwenye muziki wa bongo fleva kwa bahati tu, kwani ni mchezaji soka mzuri sana na ilikuwa asajiliwe na moja kati ya timu ya Ligi Kuu Tanzania Bara.

Hata hivyo alikuwa anajishughulisha na muziki wa kizazi kipya na tayari alikuwa amesharekodi ngoma ya 'Cinderella' iliyompa umaarufu na kuamua kuachana na soka, ingawa pia aliwahi kuichezea Coastal Union kwenye Ligi Kuu Tanzania Bara, misimu miwili iliyopita.

**Banana Zorro**

Huyu si msanii tu, ila ni mwanamuziki pia. Ana uwezo wa kupiga muziki laivu ukiwa unapigwa vyombo jukwaani, kitu ambacho si wasanii wengi wanakiweza.

Inawezekana kwa sababu baba yake ni mwanamuziki mkongwe na maarufu nchini, Zahir Ally Zorro aliyewahi kupiga bendi mbalimbali, zikiwemo JKT Mafinga maarufu kama 'Kimulimuli', Sambulumaa, Washirika Tanzania Stars na nyingine nyingi.

Banana ambaye kwa sasa ana bendi yake ya muziki, ni mmoja wa wasanii wachache nchini wanaotumia majina yao halisi.

**Vanessa Mdee**



Anajitambulisha kwa majina yake yote mawili. Na hata mashabiki wake wanamfahamu kwa majina yake yote. Ukimuuliza mtu msanii 'Vanessa'. Atakuuliza tena Vanessa Mdee?

Imedhihirika kuwa licha ya wasanii wengi duniani kuwa na majina yasiyo halisi. Lakini wasanii wa kike ndiyo wanaongoza kwa majina ya kubuni. Lakini hili siyo kwa msanii huyu. Amekuwa mahiri pia kwenye muziki kiasi cha kujipatia umaarufu mkubwa.

**Aslay Isihaka**

Jina lake halisi ni Aslay Isihaka Nassor. Mwanzoni alijiita Dogo Aslay. Jina ambalo pia halikupindisha jina lake halisi. Na hata sasa ameendelea kujitambulisha kwa jina lake.

Mmoja wa wasanii vijana kabisa ambao wamekuwa mastaa akiwa wa umri mdogo.

**Mrisho Mpoto**

Ni mwimbaji, mtunzi na mshairi. Ana aina yake ya staili ya uimbaji wake ambao ni wa kughani mashairi. Amejipatia umaarufu mkubwa kutokana na aina yake hii ya muziki ambao maneno na ujumbe wake unafikirisha zaidi kuliko kukupa burudani ya kucheza.

Kutokana na aina yake ya muziki, muonekano, mavazi yake, na hata staili yake ya maisha, wala isingekuwa rahisi kwake kutumia jina la kubuni na kuachana na jina lake halisi.

Ni kwa sababu yeye mwenyewe ni muumini wa utamaduni wa Mwafrika na maisha ya asili.



# Gold pole kuishi na seli mundu

MWANAMUZIKI nyota wa Nigeria, Adekunle Gold, ametoboa siri ya maisha yake baada ya kueleza ana matatizo ya seli mundu.

Akitumia ukurasa wake wa Instagram, Gold aliwaambia wafuasi wake kwamba amezaliwa akiwa na ugonjwa huo na anaendelea kuishi nao.

"Najisikia mpambanaji na hatimaye nitaweza kuwa na wewe sehemu ya maisha yangu, mwishowe nitaweza kusema ukweli wa maisha yangu kuwa naendelea kuishi na seli mundu," amesema.



## Hongera Tiwa Savage

MSANII wa muziki wa Nigeria, Tiwa Savage, amefanikiwa kuongeza elimu baada ya kutunukiwa cheti cha shahada ya uzamivu.

Savage amesoma katika chuo kikuu cha Kent nchini Uingereza.

Mwanamuziki huyo ambaye ni mama wa mtoto mmoja alitunukiwa cheti cha udaktari wa mambo ya fedha katika sherehe zilizofanyika katika chuo hicho hivi karibuni.

## Cannon umezidi sasa

MWIGIZAJI wa Marekani na mtangazaji wa TV, Nick Cannon amefichua kuwa huenda akawa na watoto zaidi mwaka huu.

Msanii huyo ambaye ni baba wa watoto wanane, alifahamisha hayo wakati akihojiwa na chombo kimoja cha habari na akaeleza furaha yake itazidi kama ataongeza watoto watatu.

Tayari mwanamitindo ambaye ana uhusiano wa kimapenzi na Cannon, Bre Tiesi ana ujauzito, huku Abby De La Rosa, ambaye ni mama wa mapacha wa Cannon pia inasemekana ana ujauzito.





## Flavour kumpoza mrembo wa Marekani

MWIMBAJI nyota wa Nigeria, Flavour amekutana na mwanamke raia wa Marekani ambaye nusura atapeliwe na mtu aliyedai kuwa yeye ndiye msanii huyo.

Wakati akihojiwa katika kituo cha MTV, mwanadada huyo alituma picha katika skrini akimuonyesha mtu anayedaiwa kutaka kumtapeli akisema yeye ndiye Flavour.

"Nimekuwa kwenye shoo ambapo shabiki yangu aliniambia kuna mtu anataka kumtapeli, nashukuru leo nipo naye tukijadiliana," amesema Flavour.

## Baba Ijesha kuozea jela

MSANII wa filamu kutoka Nollywood Olanrewaju Omiyinka, maarufu kama Baba Ijesha amehukumiwa kifungo cha miaka kumi na sita jela.

Hakimu Oluwatoyin Taiwo wa Mahakama ya Unyanyasaji wa Nyumbani na Makosa ya Kijinsia ya Ikeja, alimhukumu mwigizaji huyo aliyefedheheka kwa kifungo baada ya kuridhika na ushahidi uliotolewa mahakamani.

Alimpata na hatia ya makosa mawili kati ya sita dhidi yake.

Baba Ijesha anatuhumiwa kumnyanyasa kingono msichana wa miaka 14 ambaye alikuwa chini ya mchekeshaji Princess.



MAKALA

## RHOBI SAMWELLY:

# Amepitia machungu ya kukeketwa, asimama kidete kuwaokoa wasichana

Na Sabato Kasika

KUNA baadhi ya wanawake waliofanyiwa vitendo vya kikatili vya ukeketaji, lakini hawako tayari kusema hadharani machungu waliyopitia.

Hata hivyo, wengi wana sababu ambazo zinawafanya wanyamaze kimya, wanahofia kutengwa na jamii iliyowazunguka endapo watakwenda kinyume na mila.

Kinyume chake, Rhobi Samwelly amesimama kidete kueleza kwamba mila hiyo yenye madhara mengi, ameipitia kwa machungu na haifai kuendelea.

Amekuwa mstari wa mbele kupiga vita ukatili huo kwa nguvu zake zote, ili kuhakikisha siku moja unakoma katika jamii yake na Tanzania kwa ujumla.

Rhobi ni mzaliwa wa Kijiji cha Kyanyari, Wilaya Butiama mkoani Mara nchini Tanzania, akiwa ni mtoto wa kwanza kuzaliwa katika familia yao yenye watoto 12.

Huyu ni Mkurugenzi wa Shirika la Matumaini kwa Wanawake na Wasichana au (Hope for Girls and Women Tanzania), lenye maskani yake mjini Mugumu.

Shirika hilo pia lina vituo vya kutunza wasichana wanaokimbia kuepuka ukeketaji kutoka nyumbani kwao katika maeneo ya Mugumu na Butiama, kwa lengo la kuwatunza.

Pamoja na uendeshaji wa vituo hivyo, Rhobi ni mke na mama wa watoto watatu, wawili ni wanawake.

Anasema haoni sababu inayomzuia kutamka hadharani kuwa amekeketwa, wakati anajua wazi kuwa ni kweli.

“Kwa nini nifiche kusema ukweli wakati nimekeketwa? Ninafanya kazi ya kupingana na vitendo hivi, kwa hiyo ni lazima niseme ukweli ili watu wajue madhara yake, kwani hata mimi yalinikuta,” anasema Rhobi.

Mkurugenzi huyo anasema, anataka jamii ambayo imekuwa ikikumbatia mila hizo, iachane nazo kwa kuwa zimepitwa na wakati na zinaweza kusababisha madhara makubwa kwa wale wanaotendewa.

Kitaaluma Rhobi ni mwalimu wa shule ya msingi aliyehitimu stashahada mwaka 1993, katika chuo cha ualimu Bunda.

Rhobi anataja msukumo wa kupambana na mila hizo kuwa ni mwaka 1984 akiwa darasa la tano, rafiki yake alifariki dunia baada ya kukeketwa na kutokwa damu nyingi, tukio hilo lilimuumiza.

“Tukio hilo limenikaa moyoni hadi leo, alikuwa mwanafunzi pekee kijijini kwetu aliyefaulu kwenda sekondari, lakini akafariki baada ya kukeketwa wakati akisubiri matokeo ya mtihani wa



darasa la saba,” anasema.

Rhobi anasema, mwaka 1986 alipohitimu elimu ya msingi, wakati anasubiri matokeo ya mtihani, mama yake alimwambia ajiandae kukeketwa, na kwamba kauli hiyo ilimwongezea machungu kwa kukumbuka yaliyomkuta rafiki yake.

Anasema, alijitahidi kupingana na mama yake kuhusu hoja ya kukeketwa, lakini mzazi wake akawa haelewi, ndipo akapata wazo la kutoroka, akaenda kwa shangazi yake kumweleza yanayoendelea nyumbani kwao.

“Cha ajabu ni kwamba shangazi aliunga mkono wazo la mama kwamba nikeketwe, majibu hayo yalinifanya nirudi nyumbani kukaa kusubiri matokeo yangu ya mtihani wa darasa la saba,” anaeleza kwa uchungu.

Anasema, siku ya kukeketwa walikusanywa wasichana 16 akiwamo yeye na mangariba wawili, lakini mmoja wao akiwa ni maalum kwa ajili yake (Rhobi), ambapo wasichana wote walifanyiwa ukatili huo.

“Juhudi zangu za kukataa ukatili huo zilikwama ndipo nikakeketwa na kuzimia kwa zaidi ya saa nne, kwani niliambiwa nilitokwa na damu nyingi, hivyo sherehe yao ya ukeketaji ikageuka kuwa huzuni,” anaongeza kusema.

Anafafanua kuwa baada ya kuzinduka alijikuta akipewa dawa za asili zikiwamo za unga, na kwamba kitendo hicho kilimzidishia machungu moyoni mwake.

Pamoja na kufanyiwa ukatili huo, wazazi wake bado walileta kikwazo kingine baada ya matokeo kutoka akiwa amefaulu kwenda sekondari, wao walitaka aolewe ili wapate mahari.

“Nilifaulu kwenda Maswa Girls Sekondari mkoani Shinyanga, lakini wao wakawa wanadai kwamba nimeshakeketwa lazima niolewe, huku baba akidai kwamba hana fedha za kunisomesha,” anasema.

Rhobi anaeleza kwamba hakukubaliana na uamuzi huo, ndipo aliporuhusiwa na kwenda kuanza kidato cha kwanza mwaka 1987 na kuhitimu mwaka 1990 na alifaulu kidato cha tano.

“Lakini nilibadilisha mwelekeo nilienda kusomea ualimu chuo cha Ualimu Bunda na kuhitimu mwaka 1993 kisha akajiunga na Jeshi la Kujenga Taifa (JKT) Buhemba mkoani Mara kwa kipindi cha miezi sita,” anasema.

### KUANZISHA TAASISI

Anasema, tangu mwaka 2017 shirika lake linaelimisha jamii kuacha ukeketaji, kwa kushirikiana na wadau mbalimbali wakiwamo maofisa maendeleo ya jamii, dawati la jinsia la polisi na wengine wanaopinga ukeketaji.

“Huwa tunafanya mikutano ya hadhara vijijini tukiwa pia na wataalam wa afya tunaosaidiana nao katika vita hii, lakini pia katika vituo vya nyumba salama, mabinti wanaelimishwa kujua madhara ya ukeketaji,” anasema.

Mkurugenzi huyo anafafanua kuwa kwa njia hiyo imekuwa ni rahisi mabinti kukimbia wanapoona wanataka kukeketwa au kutoa taarifa kwenye vyombo vya dola,ili hatua za kisheria zichukuliwe dhidi ya wahusika.

Anaeleza mabinti ambao ni wanafunzi wanaofika katika vituo hivyo, hutafutiwa shule za jirani ili kuendelea na masomo, huku wengine ambao hawasomi huwa wanafundishwa ufundi ukiwamo wa kushona nguo.

“Yaani tangu mwaka 2017, mabinti wengi waliopitia nyumba salama, wamefundishwa ujuzi mbalimbali ukiwamo wa kushona, na wengine wameanza kujitegemea,” anasema.



Mkurugenzi huyo anafafanua kuwa wasichana waliopo katika nyumba salama za shirika hilo kwa sasa ni 127, kati ya hao 68 wako Mugumu na Butiama 59.

### UKUBWA WA TATIZO NCHINI

Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum, Dk.Dorothy Gwajima, anasema mmoja kati ya wanawake 10 wenye umri wa miaka 15 hadi 49 nchini, amekeketwa.

Hata hivyo, anasema hali ya ukeketaji imekuwa ikipungua kutokana na jitihada za serikali, asasi za kiraia na wadau wengine wanaoshiriki kutokomeza na kubadili mitazamo ya jamii kuhusu mwanamke na mtoto wa kike.

“Lakini kuna mikoa ambayo takwimu za ukeketaji bado ziko juu, ikiwamo Manyara asilimia 58, Dodoma asilimia 47, Arusha asilimia 41 na Mara asilimia 32 ,” anasema Dk. Gwajima.

Waziri anasema, vita dhidi ya ukatili ukiwamo ukeketaji nchini, inatakiwa kuhusisha watu wa kanda zote, ili kuleta mafanikio yaliyokusudiwa, ikiwa ni pamoja na kuwabaini na kuwasaidia manusura wa ukeketaji katika jamii.

“Aidha, serikali imetunga na kuzifanyia maboresho sheria mbalimbali ili kuimarisha ulinzi wa wanawake na watoto nchini kutokana na vitendo vya ukatili ikiwamo ukeketaji,” anasema.

Inaelezwa kuwa vitendo hivyo vinakwamisha utendaji kazi wa asili wa mwili wa mwanamke na kuna madhara makubwa kiafya na kisaikolojia kwa wanawake.

Daktari Majaliwa Marwa kutoka Shirika la Kimataifa la masuala ya Afya ya Uzazi na Idadi ya Watu Duniani (UNFPA) Tanzania, anataja madhara ya muda mfupi kuwa ni kifo kutokana na kutoka damu nyingi na maumivu makali.

“Uharibifu mkubwa wa mfumo wa nje wa viungo vya uzazi na maambukizi, na madhara ya muda mrefu ni maumivu makali ya muda mrefu, maambukizi ya mara kwa mara ya njia ya mkojo,” anasema Dk.Marwa.

Dk. Marwa anataja madhara mengine ni kupungua kwa raha ya kujamiiana na msongo wa mawazo utokanao na maumivu.

“Vilevie kuna kuongezeka kwa hatari za kujifungua kwa njia ya upasuaji, kuongezeka vifo vya uzazi, kuongezeka hatari za vifo vya watoto wachanga, kuongezeka kwa hatari ya watoto kuzaliwa kabla ya muda,” anasema.

Anasema, aliyekeketwa anaweza kutokwa damu nyingi wakati na baada ya kujifungua au watoto kuzaliwa na uzito mdogo (njiti), lakini pia kupata madhara zaidi katika njia ya mkojo kwa wagonjwa wenye fistula.

MAKALA

TULIKOTOKA, TULIPO & TUNAKOKWENDA...

# Mtu kugeuka chatu kulivyotikisa nchi

## ●Kiwewe kila kona, hadi polisi
## ●Kisa, dawa ya mapenzi 'limbwata'



**Na Adam Fungamwango**

ILIKUWA ni patashika nguo kuchanika kwa wakazi wa jiji la Dar es Salaam wakati huo. Hakukuwa na mitandao ya kijamii kama sasa wala simu, lakini taarifa zilienea kila kona.

Umati wa watu ulifurika kutoka kila kona jijini Dar es Salaam kushuhudia tukio hilo. Tukio la binadamu kugeuka chatu.

Akinababa walitembea kwa miguu, wengine kupanda basi, akinamama khanga mkononi, na watoto hawakukosekana, wakamiminika eneo la Buguruni kujionea wenyewe.

Pata picha, watu wanakimbilia kwenda kuangalia mtu ambaye inasadikiwa amegeuka kuwa chatu.

Walioeneza habari hiyo walidai kuwa, mtu huyo mwili wake ndiyo umegeuka chatu, lakini kichwa na sura imebaki kuwa ya binadamu.

Tangu habari hizo zilivyoenea watu toka kila pembe walizidi kumiminika na kuifanya Buguruni yote kuelemewa na ugeni kiasi sasa ikawa si ugeni tena, bali ni fujo.

Tukio hili la aina yake litakalobaki kuwa historia si Dar es Salaam tu, bali nchini Tanzania lilitokea mwaka 1987, wakati zilipoenea habari za mtu, au binadamu kugeuka chatu maeneo ya Buguruni. Ni habari iliyoenea kwa haraka kama moto kwenye nyasi za nyika wakati wa kiangazi.

Cha ajabu wakati huo hakukuwa na mitandao ya kijamii wala simu kama sasa, lakini watu walipashana taarifa na kuenea haraka sana.

Kama kawaida ya taarifa za kupeana, kila anayempatia mwenzake, naye anamsimulia mwenzake kwa namna ambayo anataka iwe nzuri zaidi kuliko aliyemhadithia mwanzo.

Kuna mtu mmoja wakati naandaa makala hii alisema siku hiyo alikuwa kwenye Uwanja wa Karume jijini Dar es Salaam, timu maarufu za Ilala zikiwa zinacheza Ligi ya Wilaya ya Ilala majira ya saa 10 jioni.

Mara taarifa hizo za mtu kugeuka chatu zikatinga uwanjani hapo. Na kwa sababu sehemu yenyewe haikuwa mbali, yaani ni Buguruni tu, dakika 15 tu uwanja ukabaki na watu wachache.

Kila mmoja alitoka kwenda kilometa chache kutoka Ilala mpaka Buguruni kuangalia tukio hilo la ajabu.

Watu walitoka Kigamboni, Kawe, Mbagala, Kongowe, Msasani sehemu ambazo kwa wakati huo zilikuwa ndiyo pembeni mwa Dar es Salaam.

Wapo pia waliotoka Mwanayamala, Kinondoni, Mburahati, Kigogo, Mabibo, Kariakoo, Magomeni, Manzese, Temeke, Tandika, Mtoni na sehemu mbalimbali za jiji kwenda Buguruni kushuhudia kwa macho yao bila kuhadithiwa.

Habari yenyewe ilikuwa inasema kuwa binadamu huyo aligeuka chatu mwili mzima na kichwa kubaki kama kilivyo baada ya kupewa dawa ya mapenzi na mkewe.

Watoa taarifa walidai, kuna mwanamke alikwenda kwa mganga wa kienyeji kutafuta dawa ya mapenzi, ambayo ni ya kumtuliza mume, kwa watoto wa mjini wanaita 'limbwata'.

Mwanamama alipewa dawa na kuambiwa nyingine amuwekee kwenye chakula na nyingine kwenye maji ya kuoga. Na kwa kufanya hivi ilikuwa ni kutaka mke apendwe zaidi na mume 'afe aoze', hata akiambiwa nini akubali tu. Pia asiwe anatoka nje ya ndoa na wanawake wengine.

Cha ajabu, ikaelezwa kwamba mara baada ya jamaa kula chakula na kuoga alibadilika kuwa nyoka aina ya Chatu na ilidaiwa alikuwa mpole na asiye na madhara yoyote. Ikasemekana baadaye askari polisi walifika na kumbeba chatu mpaka kwenye kituo cha polisi Buguruni.

Wasimualiaji wengine wakadai kuwa, jamaa aliingia bafuni, akamwagia kopo la kwanza, la pili, la tatu akageuka chatu.

Wapo walioenda mbali zaidi na kudai mke aliipata dawa hiyo kutoka kwa mganga mmoja kutoka Msumbiji, lakini wakatetea kuwa hakumloga kwa nia mbaya, alitaka kulikoleza penzi lao tu, lakini mambo yakaharibika.

Askari mmoja wa kituo cha Polisi Buguruni ambaye kwa sasa amestaafu, alisema siku ya tukio alikuwepo kazini na wenzake.

Alisema aliona kundi la watu likivamia kwenye kituo. Hata wao walishtuka na kushangaa kuna nini, lakini wakasikia wananchi wakipiga kelele wakitaka atolewe huyo mtu anayegeuka chatu.

Mmoja wa watu waliopita eneo hilo siku hiyo aliniambia wakati huo alikuwa anasoma shule ya msingi na alibahatika kuuona umati huo

"Nilikuwa natoka shule, nilibahatika kuuona ule umati kituo cha polisi Buguruni uliokuwa ukitaka kumuona chatu mtu, bahati mbaya nilikuwa kwenye daladala nikashindwa kuteremka kwenda kuona kwa sababu sikuwa na nauli nyingine." Alisema.

Wengi waliamini na hata leo bado wanaamini kuwa lilikuwa tukio la kweli. Lakini wengine hawakuamini na wanaendelea kutoamini hadi sasa.

Pamoja na stori yote hii, hadi leo hakuna hata mtu mmoja aliyewahi kusema kuwa amemuona huyo chatu kwa macho.

Wengi wamekuwa wakilielezea tukio kwa ujumla. Wanasema kuwa watu wamemuona. Kutokana na hali hiyo tukio hilo linabaki kuwa ni la uvumi kuliko uhalisia.

Askari polisi huyo mstaafu anathibitisha kuwa hawajawahi kwenda popote kumchukua binadamu aliyegeuka chatu na kwamba waliposikia wananchi wakitaka atolewe huyo mtu anayegeuka chatu, wakidai ameletwa hapo, walishangaa kwani hakukuwa na kitu kama hicho na hawajui uvumi huo ulianzia wapi na kwa nini.

Kutokana na umati kuwa mkubwa na kuongezeka kila sekunde ilivyozidi kwenda mbele anasema ilibidi ulinzi uongezwe na kutawanya watu, na hiyo ilifanywa na kikosi cha mbwa na farasi kilichokuwa kinalinda usalama kwenye mechi Uwanja wa Karume, ambacho kwa kiasi kikubwa ndicho kilichofanikiwa kusambaratisha umati ule kituoni na maeneo mengine Buguruni kwani watu walikuwa wengi sana.

Zaidi ya mwezi mzima eneo hilo lilibaki kwenye doria, kwani bado watu walikuwa wakifika kuangalia nini kinaendelea.

Huu unabaki kuwa ndiyo uvumi mkubwa zaidi kuwahi kutokea kwenye historia ya nchi hii.

Ni kwa sababu ulienea nchi nzima na hata waliokuwa wanatoka mikoani hata baada ya miaka kadhaa, walitaka wenyeji wao wawapeleke Buguruni, wakaone eneo ambalo ilisemekana mtu kageuka chatu. Nimesema kuna watu hadi leo wanaamini kuwa ni kweli. Buguruni ikawa ni eneo maarufu zaidi.

Haijulikani na nani au kina nani waliokuwa nyuma ya huu uvumi, ambao ulitungiwa nyimbo nyingi kwenye ngoma mbalimbali za asili, hasa mdundiko ambao wakati huo ulikuwa maarufu sana Dar.

Ni uvumi mkubwa zaidi hadi leo hii, unaozidi hata ile ya 'Simba Kidawa' ambayo haitofautiani na huu, ambao ulidai mwanamke aliyekuwa akigeuka simba anaposhuka juu ya kichuguu, lakini akipanda anakuwa binadamu. Ni mambo kama haya ya dawa za mapenzi.

Ulizidi hata ule wa wezi kujifanya wafu kule Kinondoni Mwembejini, wakitoka makaburini na shuka nyeupe, wakaingia kwenye baa na kujifanya ni marehemu waliofufuka, hivyo wateja na watu wa kaunta kukimbia.

Ni uvumi mkubwa zaidi kutokea kuliko ule wa wapenzi 'kung'anganiana'. Ukaushinda hata ule wa miaka ya hivi karibuni wa dereva kugeuka manyoya baada ya kupeana mikono na mtu aliyekuwa nje ya gari maeneo ya daraja la salenda, ikielezwa kuwa polisi wakalichukua gari na kuliweka kwenye kituo cha polisi cha hapo, kabla ya Jeshi la Polisi kukanusha uvumi huo.

**Tuma meseji 0714 350534**

## Sri Lanka yapata Waziri Mkuu

**COLOMBO, Sri Lanka**

RAIS mpya wa Sri Lanka Ranil Wickremesinghe, amemteua mshirika wa kisiasa wa aliyekuwa kiongozi wa nchi hiyo aliyekimbia uhamishoni, Gotabaya Rajapaksa, kuwa waziri mkuu mpya.

Uteuzi huo umefanywa saa chache tu baada ya wanajeshi na polisi kulivunja kwa nguvu eneo kuu la maandamano lililokaliwa kwa miezi kadhaa na waandamanaji waliokuwa na hasira dhidi ya serikali.

Raia wa nchi hiyo wamekasirishwa kutokana na kuporomoka kwa uchumi.

Uvamizi huo ulifanywa usiku wa juzi ingawa waandamanaji walikuwa wametangaza kuwa wangeondoka jana kwa hiari.

Marekani na Umoja wa Mataifa na wengine wamelaani matumizi ya nguvu kupita kiasi.

Wickremesinghe alichaguliwa na wabunge kuwa rais mpya na amemteua Dinesh Gunawarde mwenye umri wa miaka 73 na anayetokea familia maarufu ya kisiasa.

Rais Wickremesinghe ametoa agizo chini ya hali ya hatari akilitaka jeshi kudumisha sheria na utulivu nchi nzima. **DW**

## Tume yakemea kukamatwa makandarasi wa uchaguzi

**NAIROBI,** KENYA

TUME ya uchaguzi nchini Kenya (IEBC) imelaani tukio la kukamatwa kwa maofisa watatu wa kampuni inayouza mifumo ya upigaji kura kwa njia ya kielektroniki kwa ajili ya uchaguzi mkuu wa mwezi ujao.

Polisi imethibitisha jana kuwa raia mmoja wa kigeni alikamatwa wakati akiwa amebeba vibandiko vya uchaguzi ambavyo havikuwa vimeidhinishwa kabla.

IEBC ilisema kukamatwa kwa maofisa hao wakuu kutoka kampuni ya Smartmatic International katika uwanja wa ndege wa kimataifa wa Nairobi ni sawa na vitisho, unyanyasaji na ulaghai.

Tume hiyo ilisema wafanyakazi hao waliokamatwa jana baada ya kuwasili kutoka Venezuela, walikuwa wamepewa kandarasi kisheria ya kusimamia miundombinu ya teknolojia ya uchaguzi kwa ajili ya uchaguzi wa Agosti 9. Msemaji wa Polisi, Bruno Shioso alisema katika taarifa kuwa polisi hawakuwa wamefahamishwa kuwa vibandiko hivyo vilikuwa vinaingizwa nchini, akiongeza kuwa havikuandamana na ofisa yeyote wa IEBC kama inavyotakiwa kisheria.

Alisema mshukiwa huyo ameachiwa huru baada ya uchunguzi.

**DW**

# Russia, Ukraine kufungua bandari

**ISTAMBUL,** UTURUKI

RUSSIA na Ukraine zinatarajiwa kutia saini mkataba wa kufungua tena shughuli za usafirishaji nafaka kupitia bandari za Ukraine zilizopo kwenye mwambao wa bahari nyeusi.

Hatua hiyo itafungua milango ya kupunguza mzozo wa upungufu wa chakula duniani.

Hayo yameelezwa na ofisi ya rais wa Uturuki, ambayo ilisema makubaliano hayo yatatiwa saini mjini Instabul katika hafla itakayoongozwa na Rais Reccip Tayyip Erdogan na kuhudhuriwa na Katibu Mkuu wa Umoja wa Mataifa Antonio Guterres na wawakilishi wa nchi hizo.

Rais wa Ukraine Volodymr Zelensky, alidokeza kuwa bandari za nchi hiyo za Bahari Nyeusi huenda zikafunguliwa hivi karibuni.

Zaidi ya tani milioni 25 za nafaka na mazao mengine zimeshindwa kusafirishwa kutokana na vita inayoendelea hali iliyosababisha kupanda kwa gharama za chakula duniani na kutishia kutokea baa la njaa kwenye mataifa mengi.

Hata hivyo hakuna maelezo ya ziada yaliyotolewa juu ya vipengele vya makubaliano hayo ya jana ambayo yatakuwa muhimu katika mustakabali wa upatikanaji chakula duniani.

Katika hatua nyingine, Wizara ya Ulinzi ya Uingereza, imechapisha ripoti mpya ya idara ya ujasusi ya nchi hiyo (MI6), ikijikita katika matumizi ya mifumo ya ulinzi ya mashambulio ya anga inayotumiwa na Russia.

Katika ripoti hiyo ilibainishwa kwamba Russia ilipeleka mifumo ya kimkakati ya ulinzi wa mashambulio ya anga aina ya S-300 na S-400 ,iliyoundwa kwa ajili ya kuangamiza makombora ya masafa marefu yanayofyatuliwa kwa ndege karibu na Ukraine tangu mwanzoni mwa uvamizi.

Silaha hizi zina mtambo mdogo kiasi kwa ajili ya kuangamiza ndege.

Mifumo hiyo inaweza kuwa tishio kwa majengo ya wazi na ya vioo, lakini hayawezi kupenya kwenye majengo imara.

Pia ilisema kuna uwezekano mkubwa silaha hizo zitakosa maeneo yaliyolengwa na kusababisha athari kwa raia kwa sababu makombora hayajatengenezwa kwa kazi hiyo na wanaoyatumia hawatakuwa wamejiandaa kwa mpango huo.

Russia imeongeza matumizi ya makombora ya ulinzi wa anga kama msaada kwa mashambulio ya ardhini kutokana na ukosefu mkubwa wa makombora ya ardhini.

Julai 21, gavana wa jimbo la Nikolaev, Vitaly Kim, alisema kwamba vikosi vya Russia vilitumia mifumo ya kukabiliana na makombora ya anga kuangamiza miundombinu, ofisi za nishati na maghala katika jimbo hilo.

Vikosi vya Ukraine vilivyoko Donbass vinaendela kuzima majaribio ya Russia kuvamia Uglegorsk TPP. Makombora ya Warussia yameendelea kujikita katika maeneo ya miji wa Kramatorsk na Seversk.

Hata hivyo, Wizara ya Ulinzi ya Russia inadai kwamba jeshi lake hulenga mashambulio yake katika vikosi vya jeshi la Ukraine.

**BBC**




Wanajeshi wa Ukraine, wakifyatua makombora kutoka mfumo wa M777 Howitzer wakiwa eneo la mstari wa mbele kujibu mashambulizi ya Russia katika mji wa Kharkiv nchini Ukraine jana. **PICHA: REUTERS**

# Kamati yamtaka Trump awajibike

**WASHINGTON,** MAREKANI

MWENYEKITI wa kamati ya Bunge la Marekani inayochunguza uvamizi uliofanywa katika majengo ya bunge amesema Rais mstaafu Donald Trump, alitumia njia ya uasi na ufisadi katika kujaribu kuyabatilisha matokeo ya uchaguzi wa 2020.

Bennie Thompson, anayewaongoza wabunge wanaochunguza shambulizi la Januari 6, mwaka jana kwenye majengo



ya Capitol, alitaka kuweko na uwajibikaji. Kauli hiyo aliitoa wakati akizungumza moja kwa moja kwenye televisheni baada ya kumalizika msururu wa vikao vya kusikiliza ushahidi kuhusu shambulizi hilo.

Wabunge wanachunguza vitendo vya Trump katika siku hiyo, ikiwemo hotuba aliyotoa karibu na Ikulu ya White House akidai kuwa uchaguzi ulikuwa umeibiwa.

Jopo hilo liliwaamuru washauri kadhaa na wasaidizi wa Trump kufika mbele yake kutoa ushahidi.

Linachunguza kama Trump au washirika wake walikuwa na jukumu katika kupanga au kuhimiza juhudi za kuzuia kuidhinishwa kwa ushindi wa Joe Biden.

Trump ambaye amedokeza kuwa anaweza kugombea tena urais mwaka wa 2024, alishitakiwa bungeni kwa mara ya pili baada ya uasi huo wa majengo ya bunge. **DW**

HADITHI

MGENI wa ajabu anatokea kwenye kijiji cha Semwanza, Lugoba mkoani Pwani. Anakotoka hakujulikani. Watu wote wanamwogopa. Ni kwa sababu hawamjui. Msichana Siwatu anajitolea kumsaidia mgeni huyo. Kwa kufanya hivyo, anabezwa kwa maneno mengi ya kejeli kwa kumsaidia mtu asiyemjua ambaye anaweza kuwa hatari kwa kijiji. Baadhi ya viongozi wa kijiji waliungana na wanakijiji kutaka wamtimue mgeni huyo asiyejulikana, lakini akakataa katakata. Pamoja na kutishwa kuwa atatengwa na kijiji, bado msichana huyo alisimama na msimamo wake ule ule wa kumsaidia kwa sababu alikuwa na shida kubwa. Matokeo ya haya, yanamuingiza Siwatu kwenye msukosuko mkubwa ambao hajawahi kuupata kwenye maisha yake kiasi cha kumkatisha tamaa. Fuatilia kisa hiki.

# KAMA IPO, IPO TU-15

**Na Adam Fungamwango**
**(0716 350534)**

**MGENI wa ajabu anatokea kwenye kijiji cha Semwanza, Lugoba mkoani Pwani. Anapotoka hakujulikani.**

**Watu wote wanamwogopa. Ni kwa sababu hawamjui. Msichana Siwatu anajitolea kumsaidia mgeni huyo. Kwa kufanya hivyo, anabezwa kwa maneno mengi ya kejeli kwa kumsaidia mtu asiyemjua ambaye anaweza kuwa hatari kwa kijiji. Baadhi ya viongozi wa kijiji waliungana na wanakijiji kutaka wamtimue mgeni huyo asiyejulikana, lakini akakataa katakata. Pamoja na kutishwa kuwa atatengwa na kijiji, bado msichana huyo aliusimamia msimamo wake ule ule wa kumsaidia kwa sababu alikuwa na shida kubwa.**

**Matokeo haya, yanamuingiza Siwatu kwenye msukosuko mkubwa ambao hajawahi kuupata kwenye maisha yake kiasi cha kumkatisha tamaa. Fuatilia kisa hiki.**

***************************************

"Hicho kitambaa sijui leso, mimi nimeshawahi kumuona nacho Maiko."

Mshtuko mkubwa ukawakumba Siwatu na Mpaje, ingawa kwa Siwatu ulikuwa mkubwa zaidi.

"Maiko huyu huyu ambaye alikuwa ananitaka akasema anataka hadi kunioa?" Siwatu akauliza kwa mshangao.

"Ndiyo huyu huyu mama. Hicho kitambaa mimi nakijua, nimeshawahi kumuona nacho si mara moja au mbili."

"Toba, kwani alikuwa anakutaka?"Mpaje akauliza.

"Siyo ananitaka tu, alimtuma huyu huyu Mage aje anibembeleze nimkubali niwe mpenzi wake, halafu baadaye anioe."

"Sasa?"

"Nikamkataa, nikamwambia siwezi kuwa naye, na wala kunioa, nikamtoa 'balu' mshenga wake huyuhuyu. Nadhani baada ya kumkataa ndiyo kanifanyia ushenzi huu, mwanaharamu mkubwa yule." Siwatu akalalamika.

"Haya shoga zangu, mimi mzigo ndiyo nimeshautua, hapa tupo watatu, yaishie hapa hapa jamani." Akaonya Mage.

"Usijali shoga, nashukuru sana kwa kunisaidia hili. Na ana bahati mshenzi huyu, ningekwenda kwa Mwenyekiti wa Kijiji hadi nyumbani kwao, lakini kwa sababu tumeambizana hapa iwe siri, basi mimi nitanyamaza."




**"Siyo hivyo Mpaje, lakini nikisema nilipokiona na kijiji hiki kikijua, mimi naweza kuwa hatarini, naweza hata kuuawa."**

"Kweli Siwatu we kuwa kimya tu, kwa sababu we hujiulizi, kwa nini wamemsema kuwa ni Bakari? Kuna namna hapo? Na kwa nini sisi tu wanawake hapa tumejua ukweli, lakini Serikali ya Kijiji imeshindwa kufanya uchunguzi na kumjua mbakaji. Kuna kitu kimepitika hapa. Tutakijua baadaye."

"Nasema hivi Mage na Mpaje, mimi namuachia Mungu, ipo siku haya yote yanaweza kufichuka."

***************************

"Kwa nini unakuwa hivyo dada yangu? Kwa nini hutaki kuolewa? Unajua kuolewa ni bahati? Katokea mtu kutoka vijiji vya mbali kidogo kuja kukuposa hutaki, unataka nini lakini?"

"Kaka sikiliza nikwambie. Kuolewa ni hiari ya mtu. Zile zama za kulazimishwa kuolewa zimepitwa. Mimi ukifika muda wa kuolewa nitaolewa. Na hata wewe hutokuja hapa kuniuliza, nitakuletea tu mtu, au mshenga atakuja kwako."

Yalikuwa ni majibizano kati ya Dibwela na dada yake Siwatu. Kaka mmoja alitoka kwenye moja kati ya vijiji vya jirani kutaka kumuoa. Alifika kwa Dibwela pamoja na mshenga wake. Habari zilipomfikia mwenyewe alikataa katakata.

Huyo anakuwa wa pili baada ya Maiko, ambaye yeye alitaka kwanza urafiki wa mtu na mpenzi wake, halafu baadaye amchumbie, lakini akakataa pia.

Ndiye huyo ambaye taarifa zinabainisha kuwa mwenye kitambaa kile kilichokutwa chini ya kitanda chake na kuamini kwa asilimia nyingi kuwa ndiye aliyembaka.

Wa pili ni huyu ambaye naye amekuja kujaribu bahati yake. Lakini wapi. Msimamo wa Siwatu unabaki pale pale hataki kuolewa.

"Unajua dada nakuonea huruma sana. Kwa lile suala ambalo limekutokea, hapa kijiji wanaume wengi wanakukwepa, kukukejeli na kukudhalilisha. Sidhani kama kuna mwanaume atakayekuja kukuoa. Hata anayependa na kutaka kukuoa, anaogopa kuchekwa na watu. Hata familia yake haitokubali mtoto wao amuoe mtu ambaye kijiji kizima kinajua nini kilitokea. Umepata huyu ambaye akikuoa, unaondoka hapa kukwepa aibu na kwenda kuishi kwingine kwa amani na utulivu." Akampasha dada yake.

"Kaka nisikilize, mimi kijiji hiki nimeshazoea kusakamwa, kumbuka nilishawahi mpaka kutengwa kabisa, sisalimiwi, nikakatazwa mpaka kuuziwa kitu chochote kwa sababu ya kumpokea Bakari mwaka jana, lakini yote yamepita. Nikaja hili nalo, nimepona, mimi nimeshazoea, wala sibabaishwi na maneno ya kijiji cha Semwanza, kwa hiyo wanicheke, wanidhalilishe, mimi poa tu. Haya yote mimi sijaomba, ni mipango ya Mungu. Kama Mungu amepanga mimi niolewe, au siku moja niondokane na hii mikosi inayonipata sawa, ila sitoishi kwa kuangalia nani anasemaje."

Maneno hayo yalimuingia Dibwela. Akanyamaza kimya. Mwanzo alionekana kutaka kuwa mkali kidogo. Lakini maelezo ya dada yake yalimfanya kuingia simanzi hasa akikumbuka jinsi alivyofiwa na wazazi wake akiwa bado mdogo.

Ingawa aliishi kwa raha kijijini hapo akipewa upendeleo maalumu, lakini kwa mwaka mmoja na kitu sasa, dada yake amekuwa akiishi maisha ya manyanyaso, shida, kubaguliwa na kila aina ya tabu.

Na mkosi kwake ulikuja baada ya kumpokea mgeni mmoja aliyeitwa Bakari mwaka mmoja na ushee uliopita. Baada ya hapo amekuwa na kila aina ya matatizo.

"Sawa dada mimi nimekuelewa. Lakini nikwambie tu kitu kimoja, ukipata mwanaume wa kukuoa, kama umempenda wewe mwenyewe niambie. huo umri uliokuwa nao ndiyo umri sahihi wa kuolewa."

"Sawa kaka, lakini nimekwambia, hakuna umri wa kuolewa ila kuna utayari wa kuolewa. Tena kuolewa na mtu ambaye umeridhika naye kaka." Akamaliza na kikao kisicho rasmi cha wanandugu hao wawili kikawa kimefungwa.

********************************

Kijiji cha Semwanza kilipokea ugeni. Watu wawili ambao hawakujulikana walipotoka, walifika kwenye ofisi za Mwenyekiti wa Serikali za Kijiji.

Walionekana kuwa na siha njema, na hawakuonekana kama wanatoka hata kwenye vijiji vya jirani, bali mjini.

Walikuwa wamevaa nguo za gharama. Mmoja alikuwa mrefu mwembamba na mwenye nywele nyingi. Mwingine ni mfupi, mnene na alikuwa na kipara.

"Karibuni wageni." Ni sauti ya mwenyekiti ikiwakaribisha.

Wakaitikia kila mmoja kivyake na kuruhusiwa kukaa.

Baada ya makaribisho na maneno ya hapa na pale, mwenyekiti akaenda moja kwa moja kwenye mada.

"Enhee wageni wangu, kwanza mmetoka wapi na niwasaidie nini?"

Mrefu akajibu "Sisi tumetoka Chalinze mjini. Nia yetu ni kumuona kijana mmoja anaitwa Dibwela."

Mwenyekiti alishituka kidogo. Jinsi walivyo na kumhitaji mwanakijiji wake Dibwela ilimshangaza.

"Vipi mnataka kukodisha shamba lake kulima?"

"Hapana, tuna mazungumzo naye." Akajibu tena yule yule.

**ITAENDELEA JUMAMOSI**

# NYONI AFUNGUKA USHINDANI WA NAMBA WAKOLEA SIMBA

**Na Adam Fungamwango**

MCHEZAJI mkongwe wa Simba, Erasto Nyoni amesema hali ya ushindani imeongezeka kwa sababu kila mchezaji anataka kupata namba katika kikosi cha kwanza kuelekea msimu mpya wa Ligi Kuu Tanzania Bara na mashindano ya kimataifa.

Akizungumza na gazeti hili kutokea Misri, Nyoni alisema mazoezi yao kwa sasa yamekuwa kama mechi, lakini kila siku zinavyozidi kusonga mbele upinzani unaongezeka kutokana na ubora wa wachezaji waliopo na kila mmoja akitaka kumshawishi Kocha Mkuu, Zoran Maki kumweka katika kikosi cha kwanza.

"Unajua kazi ni kazi, timu hii ina wachezaji wazuri, kwa hiyo ushindani lazima uwepo na unapokuwa ushindani ndipo kunapokuwa na mafanikio. Kila mmoja anahitaji kucheza kwenye timu hii ndiyo maana unaona watu wanapambana, kazi atakuwa nayo kocha, yeye ndiye ataamua," alisema Nyoni.

Mchezaji huyo anayeweza kumudu nafasi zote za nyuma, ikiwa ni pamoja na kiungo mkabaji alionekana kufurahishwa na mazingira yaliyopo katika mji huo, vikiwamo vyakula pamoja na viwanja vya kufanyia mazoezi.

"Yaani hapa masuala ya chakula, sana tu, tunafanya kazi ngumu, kwa hiyo lazima tule vizuri kwa hiyo tunakula mpaka basi tu, mazingira mazuri, viwanja tunachagua leo tuchezee hiki, kesho tunachezea kile, yaani kila siku tunaamua tucheze kiwanja gani, kuna viwanja kibao hapa, yaani kule nyumbani tungekuwa na viwanja vingi na bora kama hivi du, sijui ingekuwaje, sijui nisemeje, lakini sisi tunainjoi huku, lakini nyumbani tunainjoi zaidi Taifa tu (Benjamin Mkapa)," alisema mchezaji huyo.

Klabu hiyo imeweka kambi katika mji wa Ismailia, ikijiandaa na msimu mpya wa ambao utafunguliwa na mechi ya Ngao ya Jamii itakayochezwa Agosti 13, mwaka huu.

Ikiwa Misri, tayari Simba iliyomaliza katika nafasi ya pili kwenye Ligi Kuu Tanzania Bara msimu uliopita, imeshacheza mechi moja ya kirafiki ya kimataifa dhidi ya wenyeji Ismailia na kutoka sare ya bao 1-1.

Kikosi cha Simba kinatarajia kurejea nchini mapema mwezi ujao kwa ajili ya kushiriki Tamasha la Simba Day ambalo litafanyika Agosti 8, mwaka huu kwenye Uwanja wa Taifa jijini Dar es Salaam.



Wasanii wa muziki wa asili wa bendi ya Mjomba wakitoa burudani katika Maonyesho ya 17 ya Vyuo Vikuu yanayofanyika kwenye viwanja vya Mnazi Mmoja jijini Dar es Salaam wiki hii. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# Ufukweni waondoka na matumaini

**Na Shufaa Lyimo**

KIKOSI cha Timu ya Soka ya Taifa ya ufukweni kimeondoka nchini jana alfajiri na kuelekea Malawi kikiwa na matumaini ya kufanya vizuri katika mechi yake ya kwanza itakayochezwa leo dhidi ya wenyeji.

Malawi itaikaribisha Tanzania katika mechi ya kusaka tiketi ya kushiriki Fainali za Kombe la Mataifa ya Afrika kwa Ufukweni (BSAFCON), huku timu hizo zikitarajiwa kurudiana Agosti 7, mwaka huu kwenye ufukwe wa Coco jijini Dar es Salaam.

Kocha Mkuu wa timu hiyo, Boniface Pawasa alisema wachezaji wote wako vizuri kiafya na kuongeza wamejipanga kurejea nyumbani na ushindi.

"Wachezaji wote wanaendelea vizuri, tunaomba Watanzania watuombee dua twende kufanya vizuri katika mchezo huo na ule wa marudiano utakaochezwa hapa nyumbani," alisema Pawasa.

Kocha huyo alisema kikosi chake kimefanya maandalizi ya muda mrefu na wamejiandaa kukabiliana na ushindani kutoka kwa wapinzani wao.

Nahodha wa timu hiyo, Jaruph Rajab alisema wachezaji wamejipanga kufanya vyema katika mchezo huo na kujiweka katika nafasi nzuri ya kusonga mbele kwenye michuano hiyo.

"Sisi kama wachezaji tumejipanga vizuri kuhakikisha tunapata matokeo mazuri katika mchezo huu, tunaomba Watanzania watuombee dua," alisema Rajab.

## KMC FC yatangaza kuendelea na Kaseja

**Na Adam Fungamwango**

KLABU ya KMC imesema haina mpango wa kumwacha golikipa wake, Juma Kaseja na kutangaza rasmi itaendelea na mkongwe huyo katika mechi za Ligi Kuu Tanzania Bara msimu ujao.

KMC pia itashiriki mashindano ya Kombe la FA ambayo bingwa wake hupata tiketi ya kuiwakilisha Tanzania Bara kwenye michuano ya kimataifa ya Kombe la Shirikisho Afrika.

Ofisa Mtendaji Mkuu wa KMC, Walter Harrison alisema Kaseja ni alama kwenye soka la Tanzania akiwa amefanya makubwa ndani na nje ya nchi, hivyo hakuna klabu yoyote anayoitumikia itataka kumpoteza.

Harrison alisema hayo kufuatia tetesi kuwa huenda klabu hiyo ikaachana na kipa huyo mkongwe aliyeanza kucheza Ligi Kuu kuanzia mwaka 2000, akiwa na klabu za Moro United, Simba na Yanga.

" Kaseja ni alama ya mpira wa Tanzania, yupo nasi kwa misimu minne sasa, amekuwa ni kama mwalimu ndani na nje ya uwanja, na kile ambacho amekifanya kwenye mpira wa Tanzania ndani na nje ya nchi, sidhani kama kuna timu inaweza kumpoteza, hatuna mpango wa kuachana naye. Bado yupo KMC sana. Hata kama hatotaka kuwa mchezaji tutamtafutia kazi nyingine, " alisema Ofisa Mtendaji Mkuu huyo.

Kuhusu maandalizi kuelekea msimu mpya, bosi huyo alisema kwa sasa wanaendelea mchakato wa kuachana na wachezaji ambao wamepata klabu nyingine, mikataba yao imeisha na pia wake inayowaacha.

Unachokiona kwenye mtandao wetu wa kijamii ni maandalizi ya msimu, hizo ni taarifa tunazowahabarisha mashabiki wetu, tunawataarifu wachezaji ambao wamepata klabu mpya, wengine mikataba imeisha na ambao tunawaacha.

"Zoezi la usajili linaendelea vizuri, hatutatangaza sasa, ila wiki ijayo tutawaweka hadharani wale wote ambao tumewasajili. Tunajitahidi kusajili timu bora ambayo itaweza kushindana," Harrison alisema.

Katika ukurasa rasmi wa instagram wa klabu hiyo umetangaza kuagana na wachezaji wake sita ambao ni Ally Ramadhani, Hassan Kessy, Sudi Dondola, Hassan Kabunda, Dennis Richard na Abbas Kapombe.

# HABARI MICHEZO

## ZISIKUPITE

### BRIGHTON YAIGOMEA CITY

OFA ya Manchester City ya pauni milioni 30 kwa ajili ya beki wa kushoto wa Timu ya Taifa ya Hispania, Marc Cucurella imekataliwa na Brighton, ambayo imetaja thamani ya mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 23 ni pauni milioni 50. (*Athletic*)

### GRIMALDO ATAJWA CITY

MANCHESTER City wamepewa ofa ya beki wa pembeni wa Benfica, Alejandro Grimaldo mwenye umri wa miaka 26, kama chaguo mbadala kwa Marc Cucurella. (*Sport*)

### LEEDS: HARRISON HAONDOKI

LEEDS United wamekataa ombi la Newcastle United la pauni milioni 18 kwa kiungo wa kati wa Timu ya Taifa ya England, Jack Harrison mwenye umri wa miaka 25. (*Football Insider*)

### EMMANUEL AWEKWA SOKONI

KLABU ya Nottingham Forest inatafuta dili la kumnunua mshambuliaji wa Nigeria, Emmanuel Dennis, huku Watford wakitaka takriban pauni milioni 25 kwa mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 24. (*Mail*)

### BARCA YAMGANDA KOUNDE

BARCELONA watafanya jaribio la mwisho kumsajili beki wa Sevilla na Timu ya Taifa ya Ufaransa, Jules Kounde, licha ya kukiri hawawezi kufikia dau la Chelsea la pauni milioni 55 kumnunua mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 23. (*Sport*)

### LAPORTE ATAJWA BARCA

BARCELONA watamgeukia beki wa kati wa Manchester City na Timu ya Taifa ya Hispania, Aymeric Laporte mwenye umri wa miaka 28, iwapo watashindwa kumsajili Jules Kounde. (*Fichajes*)

### UNITED, CHELSEA VITANI

MANCHESTER United na Chelsea wanashindana kumsajili beki wa Bayern Munich na Timu ya Taifa ya Ufaransa, Benjamin Pavard mwenye umri wa miaka 26. (*L'Equipe, via Sun*)

### DORTMUND YAMTAKA SUAREZ

KLABU ya Borussia Dortmund inafikiria kumnunua mshambuliaji wa Timu ya Taifa ya Uruguay, Luis Suarez mwenye umri wa miaka 35, baada ya mkataba wake na Atletico Madrid kumalizika msimu huu. (*Sky Sports*)

### CHELSEA MAMBO MAGUMU

CHELSEA wanatatizika kuwasilisha ombi la kutaka kumnunua mlinda mlango wa Hispania, Kepa Arrizabalaga mwenye umri wa miaka 27, na mshambuliaji wa Ujerumani, Timo Werner (26), kwa sababu ya madai yao ya mshahara. The Blues pia wanapata mgumu wa kuwaondoa wachezaji kama mshambuliaji wa Ubelgiji, Michy Batshuayi (28), na kiungo wa kati wa England, Ross Barkley (28). (*Telegraph*)

### CHUKWUEMEKA NJIA MOJA

KIUNGO wa kati wa Aston Villa na England aliye chini ya umri wa miaka 19, Carney Chukwuemeka hana nia ya kusaini mkataba mpya pale Villa Park, huku Barcelona na Borussia Dortmund wakifuatilia hali ya mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 18. (*Sky Sports*)

### PSG KUMUUZA WIJNALDUM

KLABU ya Paris St-Germain imewapa Roma nafasi ya kumsajili kiungo wa kati wa Timu ya Taifa ya Uholanzi, Georginio Wijnaldum mwenye umri wa miaka 31. (*Corriere dello Sport*)

# DONDOO ZA SOKA
## MAGAZETI YA ULAYA




# MANE MWANASOKA BORA WA AFRIKA MWAKA 2022

**●●● Aongoza tuzo tano zilizokwenda katika taifa la Senegal katika sherehe za CAF...**

**RABAT,** MOROCCO

SADIO Mane wa Senegal ametwaa tuzo ya mwanasoka bora wa mwaka wa Afrika kwa mara ya pili mfululizo katika hafla ya utoaji wa tuzo za Shirikisho la Soka Afrika (CAF) zilizofanyika usiku wa kuamkia jana katika mji mkuu wa Morocco, Rabat.

Mane alifunga penalti ya ushindi wakati Senegal ilipoilaza Misri katika hatua ya matuta kwenye fainali ya Kombe la Mataifa ya Afrika (AFCON 2022) na kulibeba kwa mara ya kwanza.

Tuzo hizo zilirejea kwa mara ya kwanza katika kipindi cha miaka mitatu baada ya kusimamishwa kutokana na janga la virusi vya corona.

**"Nina furaha sana sana kupokea kombe mwaka huu," alisema Mane mwenye umri wa miaka 30 mara baada ya kupokea zawadi yake.**

Mane alimshinda golikipa wa Chelsea, Edouard Mendy na mchezaji mwenzake wa zamani pale Liverpool, Mohamed Salah, ambaye timu yake ya Misri ilipoteza fainali hiyo ya Februari mwaka huu.

Tuzo ya Mane ilikuwa kati ya tano zilizonyakuliwa na Senegal katika jumla ya vitengo saba vya wanaume baada ya usiku wa kukumbukwa kwa taifa hilo la Afrika Magharibi.

Kocha wa muda mrefu wa Senegal, Aliou Cisse alishinda kocha bora wa mwaka, huku timu yake ikichaguliwa kuwa timu bora ya mwaka ya wanaume.

Pape Sarr alichaguliwa kuwa mchezaji bora chipukizi wa mwaka na Msenegal mwingine, Pape Ousmane Sakho, akishinda tuzo ya bao bora la mwaka ambapo anaichezea klabu ya Simba ya Tanzania.

BREAKING NEWS

SUPA JACKPOT KWA 1000/- 1,016,4

MECHI KALI

ASTON VILLA
VERSUS
MANCHESTER UTD

1 | 3.45
X | 3.70
2 | 1.85

KUWEKA PESA:
- PIGA *150*87#, CHAGUA 4
- WEKA PESA.

tigo pesa vodacom m-pesa halopesa airtel money ZANTEL EZYPESA

SEND

SportPesa

SPORTPESA.CO.TZ

PIGA *150*87#

GBT:0249 HUDUMA KWA WATEJA MASAA 24, PIGA:
0764115588, 0677115588
0685115588

18+

@TZSportPesa @SportPesaTZ @tzsportpesa

# LINGARD ASAJILIWA NOTTINGHAM FOREST



**LONDON, England**

JESSE Lingard amechagua kujiunga na Nottingham Forest kwa kusaini mkataba wa mwaka mmoja na klabu hiyo iliyopanda daraja kucheza Ligi Kuu England msimu huu.

Lingard mwenye umri wa miaka 29, aliondoka Manchester United msimu huu wa joto baada ya kumalizika kwa mkataba wake, akichagua kutoongeza muda wake kwa sababu ya kukosa nafasi ya kucheza kwa Mashetani Wekundu hao.

Kiungo huyo mshambuliaji aliibukia kwenye akademi ya United na kucheza mechi 232 katika mashindano yote, akifunga mabao 35.

Katika msimu wake wa mwisho pale Old Trafford, Lingard alicheza mechi 16 pekee za Ligi Kuu England kwa jumla ya dakika 367.

Hapo awali alikuwa amefunga mara tisa katika kipindi cha mkopo cha michezo 16 akiwa na West Ham msimu wa 2020-21.

Hata hivyo, Forest imewashinda wapinzani wao kwa kuripotiwa kumpa kiungo huyo aliyeichezea England meshi 32 mshahara wa pauni 200,000 kwa wiki.

# Werner mambo magumu Chelsea

**LONDON, England**

CHELSEA wanatatizika kuwauza, Kepa Arrizabalaga mwenye umri wa miaka 27, na mshambuliaji wa Ujerumani, Timo Werner (26), kwa sababu ya madai yao ya mshahara.


The Blues pia wanapata ugumu wa kuwaondoa wachezaji kama vile mshambuliaji wa Ubelgiji, Michy Batshuayi mwenye miaka 28 na kiungo wa kati wa England, Ross Barkley (28).

Kwa mujibu wa The Telegraph Werner na Kepa ni miongoni mwa wachezaji wenye mahitaji ya mishahara mikubwa.

Mlango wa uhamisho hapo Stamford Bridge unaweza kwenda taratibu kutokana na mishahara mikubwa wanayolipwa wachezaji wa Ligi Kuu England kati ya ligi tano kubwa Ulaya.

Klabu za Ligi Kuu England zinaongoza kwenye orodha ya wachezaji wanaolipwa mishahara mikubwa kwa soka la Ulaya na tangu ilipochukuliwa na Roman Abramovich, Chelsea imekuwa ikinunua wachezaji wakubwa maarufu.

Kubadilika kwa soko msimu huu limekuwa jambo gumu kwa Chelsea kuuza wachezaji.



## HABARI MICHEZO

-28,582/-

# TAMWA YALALAMIKIA UTEUZI KAMATI MDUNDO WA TAIFA

**Na Romana Mallya**

CHAMA cha Wanahabari Wanawake Nchini (TAMWA) kimesikitishwa na uteuzi usiozingatia usawa wa jinsia katika Kamati ya Kuratibu Mdundo wenye asili ya Tanzania pamoja na ile ya kuratibu vazi la taifa.

Kauli hiyo imekuja siku moja baada ya Waziri wa Utamaduni, Sanaa na Michezo, Mohamed Mchengerwa kutangaza kamati hiyo ya kuratibu mdundo baada ya ile ya awali ya vazi la taifa.

Taarifa ya TAMWA iliyotolewa imesema, miongoni mwa wajumbe tisa wa kamati hiyo, kuna uwakilishi wa mwanamke mmoja, Fatuma Hassan maarufu kama DJ Fetty.

Ilisema katika taarifa iliyotolewa juzi na kusainiwa na Mkuu wa Kitengo cha Mawasiliano Serikalini, John Mapepele, ilieleza waziri huyo ameteua kamati hiyo itakayoratibu upatikanaji wa mdundo wenye asili ya kitanzania.

"Hivi karibuni waziri ameteua kamati maalum ya kuratibu vazi la taifa, ambayo ina mwenyekiti na katibu, wote wanaume na wajumbe watano kati yao, mwanamke ni mmoja ambaye ni mwanamitindo, Khadija Mwanamboka," ilisema taarifa hiyo.

Taarifa hiyo ilisema siyo kwamba TAMWA inakosoa ubora na weledi wa wajumbe na viongozi wa kamati hiyo, bali chama hicho ni chombo ambacho kina wajibu wa kutetea ushiriki wa wanawake katika uongozi na uamuzi.

"Kimesikitishwa na uteuzi huu ambao haujazingatia usawa wa kijinsia. TAMWA inaamini kuwa kuna wanawake lukuki wenye ujuzi, ujasiri na wenye kazi za kupigiwa mfano katika sekta ya sanaa na utamaduni ambao wangeweza kutimiza majukumu yaliyoainishwa na wizara katika kamati hizi," ilisema.



Wanafunzi wa Shule ya Msingi Kisemvule wakicheza mpira wakati wa mapumziko kwenye viwanja vya shule hiyo iliyopo Mkuranga mkoani Pwani juzi. **PICHA : JUMANNE JUMA**

# Bagamoyo Marathon yanukia

**Na Moshi Lusonzo**

WANARIADHA zaidi ya 2000 wanatarajia kushiriki mbio za Bagamoyo Historical Marathon zilizopangwa kufanyika Julai 31, mwaka huu.

Mkurugenzi wa Kampuni ya 4Beli, Dominic Mosha alisema maandalizi yanakwenda vizuri na tayari wanariadha zaidi ya 1,000 wameshajiandikisha kushiriki mbio hizo zitakazofanyika mkoani Pwani.

Mosha alisema mbio hizo zitaanzia katika Uwanja wa Shule ya Mbaruku na kuzunguka kwenye maeneo mbalimbali ya kihistoria katika mji huo mkongwe na kumalizika kwenye eneo hilo.

Alisema lengo la mbio hizo ni kuutangaza mji huo wa kitalii na kuunga mkono juhudi za Rais, Samia Suluhu Hassan kuongeza watalii kwenye vivutio mbalimbali nchini kupitia filamu ya Tanzania Royal Tour.

Aliongeza wanariadha watakaoshiriki watachuana katika umbali wa kilomita 21, kilomita 10 kwa makundi maalumu ya makampuni na taasisi, kilomita 10 kwa mtu mmoja mmoja na kilomita tano kwa watu mchanganyiko.

Alitaja zawadi kwa mshindi wa kwanza upande wa wanawake na wanaume kwa mbio za nusu marathon ni Sh. milioni moja, mshindi wa pili Sh. 750,000 na mshindi wa tatu Sh. 500,000 huku Sh. 500,000 itatolewa kwa washindi wa mbio za kilomita tano na ada ya ushiriki ni Sh.30,000.


SUPA JACKPOT

MECHI WIKI HII

BASHIRI KWA USAHIHI MECHI ZOTE

| TAREHE | MUDA | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 01. 23/07/22 | 19:15 | Kortrijk vs OH Leuven | 2.39 | 3.48 | 2.79 |
| 02. 23/07/22 | 21:30 | Hannover vs St. Pauli | 2.38 | 3.43 | 2.83 |
| 03. 23/07/22 | 21:30 | Sarmiento vs Colon Santa Fe | 2.42 | 3.14 | 3.14 |
| 04. 23/07/22 | 22:30 | Vila Nova GO vs Vasco da Gama | 2.63 | 2.73 | 3.08 |
| 05. 24/07/22 | 00:30 | Nautico PE vs Londrina PR | 2.30 | 2.97 | 3.36 |
| 06. 24/07/22 | 02:30 | CRB AL vs Novorizontino SP | 2.48 | 2.93 | 3.08 |
| 07. 24/07/22 | 02:30 | FC Cincinnati vs Nashville | 2.32 | 3.42 | 3.02 |
| 08. 24/07/22 | 02:30 | Orlando City vs Philadelphia Union | 2.37 | 3.43 | 2.93 |
| 09. 24/07/22 | 03:00 | Botafogo RJ vs Atletico Pr | 2.30 | 3.33 | 3.03 |
| 10. 24/07/22 | 03:00 | DC United vs Montreal Impact | 2.31 | 3.38 | 3.07 |
| 11. 24/07/22 | 03:30 | Sporting Kansas City vs Los Angeles FC | 2.90 | 3.50 | 2.35 |
| 12. 24/07/22 | 05:00 | Vancouver Whitecaps vs Chicago Fire | 2.28 | 3.45 | 3.05 |
| 13. 24/07/22 | 12:00 | Tokyo Verdy vs Yokohama | 2.90 | 3.30 | 2.42 |
| 14. 24/07/22 | 14:30 | Karlsruher SC vs Magdeburg | 2.50 | 3.40 | 2.70 |
| 15. 24/07/22 | 17:00 | Mechelen vs Royal Antwerp | 2.55 | 3.40 | 2.65 |
| 16. 24/07/22 | 22:00 | Westerlo vs Cercle Brugge | 2.68 | 3.28 | 2.58 |
| 17. 24/07/22 | 22:00 | Juventude RS vs Ceara CE | 2.58 | 2.98 | 2.93 |

MECHI ZA USHINDI

"1" NI TIMU YA NYUMBANI KUSHINDA "X" NI TIMU KUTOKA SARE "2" NI TIMU YA UGENINI KUSHINDA.

JUMAMOSI - 23/07/2022

| MUDA | GAMEID | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 12:45 | 2730 | Aston Villa vs Manchester Utd | 3.45 | 3.70 | 1.85 |
| 13:00 | 1516 | Urawa Red Diamonds vs Paris St Germain | 9.59 | 6.80 | 1.18 |
| 14:00 | 2123 | Ilves Tampere vs HJK Helsinki | 4.03 | 3.49 | 1.77 |
| 14:00 | 2386 | Nurnberg vs Greuther Furth | 2.42 | 3.36 | 2.71 |
| 14:00 | 2565 | Holstein Kiel vs Kaiserslautern | 2.13 | 3.36 | 3.21 |
| 14:00 | 5726 | Bucheon vs Chungnam Asan | 2.84 | 3.04 | 2.39 |
| 15:00 | 4119 | CSKA Moscow vs Sochi | 2.16 | 3.34 | 3.14 |
| 16:00 | 1318 | Shamrock Rovers vs Drogheda Utd | 1.17 | 5.88 | 13.73 |
| 16:00 | 4579 | Ajax vs Eintracht Frankfurt | 1.52 | 4.52 | 4.52 |
| 16:00 | 4753 | IK Brage vs Halmstads BK | 3.36 | 3.36 | 2.16 |
| 16:00 | 5123 | Malmo vs Sirius FK | 1.28 | 5.12 | 8.08 |
| 17:00 | 1409 | PK-35 vs EIF Ekenas | 2.17 | 3.39 | 2.90 |
| 17:00 | 2686 | Rangers vs Tottenham | 3.67 | 3.72 | 1.79 |
| 17:00 | 3130 | Charleroi vs Eupen | 1.69 | 3.88 | 4.43 |
| 17:00 | 3393 | Bodo Glimt vs Jerv | 1.14 | 7.81 | 14.02 |
| 17:00 | 4770 | AC Oulu vs IFK Mariehamn | 2.32 | 3.20 | 2.80 |
| 17:00 | 5014 | Pif Jalkapallo vs IF Gnistan | 3.58 | 3.68 | 1.82 |
| 17:00 | 5140 | Pepo Lappeenranta vs TPS Turku | 6.67 | 4.51 | 1.37 |
| 17:00 | 5660 | VPS Vaasa vs Haka | 2.43 | 3.29 | 2.60 |
| 17:30 | 2529 | Gazovik Orenburg vs Ural Yekaterinburg | 2.35 | 3.05 | 3.05 |
| 18:00 | 1877 | LASK Linz vs Austria Klagenfurt | 1.36 | 4.71 | 6.48 |
| 18:00 | 3412 | Liebherr Gak vs Floridsdorfer AC | 2.65 | 3.34 | 2.36 |
| 18:00 | 4442 | SKN St Polten vs Dornbirn | 1.43 | 4.52 | 5.50 |
| 18:30 | 2901 | Cracovia vs Korona Kielce | 1.57 | 3.73 | 5.11 |
| 18:30 | 4342 | Mjallby vs Degerfors | 1.71 | 3.53 | 4.32 |
| 18:30 | 5547 | Beroe vs Lokomotive Sofia | 1.79 | 3.34 | 4.13 |
| 19:00 | 2411 | Slovan Bratislava vs AS Trencin | 1.45 | 4.40 | 5.48 |
| 19:00 | 2904 | Rosenborg vs Tromso | 1.91 | 3.51 | 3.76 |
| 19:00 | 2929 | Liptovsky Mikulas vs Zemplin Michalovce | 2.37 | 3.30 | 2.66 |
| 19:00 | 3004 | Lietava Jonava vs Futbolo Akademija Siauliai | 14.66 | 7.43 | 1.11 |
| 19:00 | 5494 | FC Zurich vs FC Luzern | 2.08 | 3.61 | 3.16 |
| 19:00 | 5916 | PSV Eindhoven vs Betis | 2.27 | 3.44 | 2.71 |
| 19:15 | 1356 | Kortrijk vs OH Leuven | 2.36 | 3.37 | 2.82 |
| 19:15 | 4759 | Zulte Waregem vs RFC Seraing | 2.22 | 3.48 | 2.97 |
| 19:30 | 4208 | Talaea El Gaish vs Misr Lel Makasa | 1.69 | 3.33 | 5.44 |
| 19:55 | 4680 | Mladost Lucani vs Red Star Belgrade | 26.43 | 8.61 | 1.06 |
| 20:00 | 1206 | FC Krasnodar vs Spartak Moscow | 2.91 | 3.36 | 2.28 |
| 20:00 | 5687 | FK Sloga Doboj vs FK Leotar Trebinje | 2.74 | 2.93 | 2.54 |
| 20:30 | 2375 | Wolfsberger AC vs Sturm Graz | 2.43 | 3.29 | 2.60 |
| 20:30 | 2688 | Voluntari vs Botosani | 2.36 | 2.95 | 3.15 |
| 21:00 | 1149 | Legia Warszawa vs Zaglebie Lubin | 1.74 | 3.54 | 4.13 |
| 21:00 | 5980 | Botev Plovdiv vs Arda Kurdzhali | 1.82 | 3.39 | 3.93 |
| 21:15 | 5834 | Maribor vs ND Gorica | 1.41 | 4.14 | 6.70 |
| 21:30 | 1526 | Hannover vs St. Pauli | 2.24 | 3.54 | 2.84 |
| 21:30 | 2714 | St. Gallen vs FC Winterthur | 1.81 | 3.91 | 3.76 |
| 21:45 | 3056 | St Truiden vs Union Saint Gilloise | 4.02 | 3.37 | 1.89 |
| 22:00 | 1321 | France W vs Netherlands W | 1.69 | 3.63 | 4.32 |
| 22:00 | 1890 | Radnik Surduluca vs FK Radnicki 1923 | 2.29 | 3.04 | 2.99 |
| 22:00 | 3050 | Partizan vs Backa Topola | 1.19 | 6.08 | 10.79 |
| 22:00 | 4153 | Slaven Belupo vs Dinamo Zagreb | 7.45 | 4.41 | 1.35 |


CHEZA KWA WAJIBU. KIWANGO CHA MAKATO YA SIMU KUZINGATIWA.

Michezo
Jumamosi Julai 23, 2022
Nipashe





Werner mambo magumu Chelsea



Kiungo mshambuliaji wa zamani wa Timu ya Soka ya Taifa ya Nigeria, Jay Jay Okcha (kushoto), akimkabidhi tuzo ya Goli Bora la mwaka ya Shirikisho la mchezo huo Afrika (CAF), mshambuliaji wa Simba raia wa Senegal, Pape Ousmane Sakho jijini Rabat, Morocco juzi. **PICHA: MTANDAO**

# SAKHO AWINDWA NA VIGOGO ULAYA

## ●●●Tuzo ya CAF yampaisha, Simba yasema haijafunga usajili, lolote linaweza...

**Na Mwandishi Wetu**

BAADA ya kutangazwa mshindi wa tuzo ya goli bora la mwaka la Shirikisho la Soka Afrika (CAF), nyota wa Simba, Pape Ousmane Sakho, ameingia katika rada za timu mbalimbali kwa ajili ya kumsajili raia huyo wa Senegal.

Goli ambalo limempa tuzo Sakho ni lile alilofunga dhidi ya ASEC Mimosas ndio limempatia ushindi huo.

Akizungumza na gazeti hili jana, Ofisa Mtendaji Mkuu wa Simba, Barbara Gonzalez, alisema wamepokea maombi kutoka katika timu mbalimbali za ndani na nje ya Afrika zikionyesha nia ya kumsajili Sakho.

Barbara alisema maombi hayo yamepelekea yeye na nyota huyo kubakia Morocco ili kufikia uamuzi juu ya ofa hizo ambazo zimejitokeza.

"Simu zimekuwa nyingi sana kwa Pape, viongozi wa Senegal waliuliza kwanini anacheza Tanzania, walikuwa wanamwambia anapaswa kuondoka sasa na ni lazima aondoke akacheze nje ya hapa," alisema Barbara.

Ofisa huyo aliongeza Simba itafanya uamuzi kwa kuzingatia malengo ya klabu lakini pia itaangalia maslahi ya mchezaji husika.

"Ukweli ni kwamba tumepokea ofa nyingi na jana (juzi) usiku baada ya tuzo watu wanatutafuta, wamemfuata mchezaji wanaomba vikao, leo (jana) wanaomba tuahirishe safari, mwisho wa siku wajibu wangu kama CEO lazima nilete kwa mabosi wangu ikiwamo mwenyekiti na rais ili maamuzi yao lazima yafanyike," Barbara alisema.

Aliongeza bado Simba haijakamilisha mchakato wa usajili kwa maana hiyo uamuzi wa mwisho wa wachezaji watakaoitumikia klabu hiyo haujafanyika huku akisema wamepokea ofa mbili zinazomhitaji, Sadio Kanoute.

"Kumekuwa na mchakato makini unaoendelea katika klabu yetu, bado hatujafunga, hatujakamilisha usajili, haijajulikana kamili nani anaingia na nani anatoka, muda ukifika tutaweka wazi, kikubwa tutazingatia malengo ya klabu tuliyojiwekea," Barbara aliongeza.

Taarifa ambazo zimepatikana jijini zinasema klabu ya zamani ya Mtanzania, Simon Msuva, Wydad Casablanca ya Morocco iko tayari kumnunua Sakho kwa dau la Sh. bilioni 1.8.

Akizungumza baada ya kukabidhiwa tuzo, Sakho aliwashukuru Watanzania, mashabiki wa Simba na wachezaji wenzake wote wa klabu hiyo.

"Asanteni Watanzania, asanteni mashabiki wa Simba, asanteni wachezaji wote, nimefurahi sana," alisema mshambuliaji huyo.

Sakho ambaye katika fainali ya kuwania tuzo hiyo alishindana na Zouhair El-Moutaraji wa Wydad na Gabadinho Mhango wa Malawi alikabidhiwa tuzo yake na mkongwe, Jay Jay Okocha.

Wakati huo huo, uongozi wa Simba jana ulimtambulisha rasmi beki wake mpya, Mohamed Outtara ambaye amejiunga na timu hiyo akitokea Al Hilal ya Sudan.

# Stars, Somalia kibaruani CHAN

**Na Saada Akida**

TIMU ya Soka ya Taifa (Taifa Stars), inavaana na wenyeji Somalia katika mechi ya kwanza ya kusaka tiketi ya kushiriki fainali za Kombe la Mataifa ya Afrika kwa Wachezaji wa Ndani (CHAN), utakaochezwa leo kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa.

Hata hivyo, Kocha Mkuu wa Taifa Stars, Kim Poulsen amelalamikia kikosi chake kutopata nafasi ya kuutumia Uwanja wa Benjamin Mkapa na badala yake nafasi hiyo ilipewa timu ya vijana U-20 ya Ufaransa (Montpellier) ambayo inajiandaa na michuano ya Cambiasso.

Poulsen alisema jana jijini maandalizi ya mechi hiyo yameendaa vizuri na wachezaji wana nafasi kubwa ya kuonyesha uwezo katika mashindano hayo ya kimataifa.

Kocha huyo alisema wanatarajia kupata matokeo chanya katika mechi hiyo ili kujiweka kwenye mazingira mazuri ya kusonga mbele katika michuano hiyo inayoandaliwa na Shirikisho la Soka Afrika (CAF).

"Lakini Stars imefanya mazoezi kwenye uwanja wa majani bandia badala ya kutumia Benjamin Mkapa, nimeshangaa kuona kuna timu (Montpellier), imeruhusiwa kutumia uwanja huo ambao timu ya Tanzania hatukutapa nafasi hiyo siku moja au mbili kabla ya mechi," alisema Poulsen.

Alisema anaamini wachezaji wake watatimiza majukumu yao kwa kuiondoa Somalia na kuikabili Uganda katika hatua ya pili na baadaye kukata tiketi ya kushiriki fainali za CHAN.

"Ukiachilia mbali wachezaji wanacheza soka la kulipwa nje akiwamo Mbwana Samatta na wengine, lakini asilimia kubwa wanaounda Stars wanacheza ligi ya ndani sasa ni jukumu lao kubeba majukumu ya wachezaji hao na kuhakikisha tunafanya vizuri na kufikia malengo," Poulsen alisema.

Nahodha wa Stars, Aishi Manula alisema licha ya kukutana na changamoto ya uwanja, wamejipanga vyema kuhakikisha wanashinda mchezo huo.

"Tunajua mchezo wetu dhidi ya Somalia utakuwa na ushindani mgumu, lakini tuna kila sababu ya kufanya vizuri, ukiangalia asilimia kubwa ya wachezaji wa Stars, tunacheza ligi ya ndani, tunaenda kupambana kuhakikisha tunashinda na kufikia malengo," alisema Manula.

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042